# Nipashe

Jumanne Aprili 20, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580556

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

ELIMU

MAUAJI CHUKI ZA MAPENZI

• Kampeni ya kitaifa kulinda uhai yaweza kuwa mwarobaini

NA CHRISTINA MWAKANGALE

"Matukio hayo ni zaidi ya mara mbili ya yaliyotokea mwaka 2020, ikilinganishwa na yaliyoripotiwa mwaka 2019

UKURASA 11

**Marekani** yamwaga vifaa kukabili corona

UKURASA 4



**Mbaroni** madai kuua mke kwa kumcharanga mapanga

UKURASA 4

# Wadai katiba mpya itawawajibisha wabunge

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**SERIKALI KUWAONDOLEA VIKWAZO WAWEKEZAJI**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wawekezaji kuendelea kuiunga mkono Serikali, huku...

UKURASA WA 3

**RAIS AFANYA ATEUZI WA VIONGOZI, BODI, TAASISI**

RAIS Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa viongozi wa bodi na taasisi mbalimbali..

UKURASA WA 7

**BIL.1.7/- KUJENGEA UWEZO WASICHANA ZATOLEWA**

UBALOZI wa Ufaransa nchini unatarajia kutoa Dola za Marekani 720,000 (sawa na Sh. Bilioni 1.7) kwa ajili ya...




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akimsikiliza mhandisi wa Kampuni ya kuunganisha magari ya GFA Vehicle Factory, Kibaha mkoani Pwani, Baraka Samson. Wa pili kulia ni Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Ally Karmali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Rais Samia kuhutubia Bunge

UKURASA 2

# Waziri Mkuu amsimamisha mkurugenzi wa fedha DART

• **Atembelea** UDA na kukuta mabasi yamenyofolewa...

*Endelea ukurasa 4*



Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi (kulia) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Bima ya Reliance Tanzania, Ravi Shankar, wakizindua rasmi huduma ya bima ya simu kwa watumiaji wa NMB Mkononi jijini Dar es Salaam. Katikati ni Kaimu Mkurugenzi wa Sheria wa Mamlaka ya Bima nchini, Emily Kiria. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store



**MICHEZO** YANGA KUMSHUSHA KOCHA WA AL MERRIK UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Wadai katiba mpya itawawajibisha wabunge

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU mbalimbali wanaofuatilia mwenendo wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wameonyesha kusikitishwa na mijadala inavyoendeshwa bungeni, huku wakisema kuna haja ya kurudi kwenye mchakato wa katiba mpya ili wananchi wawe na mamlaka ya kuwawajibisha au kuwaondoa wabunge wanaoshindwa kuwajibika.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe, wadau hao walisema kwa sasa wanachoshuhudia kwa wabunge ni kusutana badala ya kujadili matatizo ya wananchi kwenye majimbo yao.

Aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Ananilea Nkya, alisema kinachotokea bungeni kwa sasa kinaonesha umuhimu wa kudai katiba mpya.

"Kinachoendelea bungeni, kinaonyesha ni namna gani kuna umuhimu na ulazima wa kurudi kwenye katiba mpya. Sidhani kama wapigakura wangekubali kuwaacha wabunge wa namna hii endapo wangekuwa na mamlaka ya kuwawajibisha," alisema Nkya.

"Wabunge wanasutana, wanajadili mtu badala wazungumze matatizo lukuki yaliyopo kwa wananchi wao ambayo ndiyo lengo la wao kuwapo humo, hii inashangaza na kusikitisha sana. Na hii ndio madhara ya kuwa na wabunge wanaosema eti wamepita bila kupingwa na wengine hawana vyama, lakini wapo tu bungeni."

Dk. Nkya alimuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati ili Bunge lirushwe mubashara na wananchi waendelee kuwapima wabunge wao ili wasirudie makosa katika uchaguzi ujao.

Pia, alishauri wananchi wajipange kuhakikisha wanafuatilia wabunge wao wanachokifanya bungeni na wanaporudi majimboni wapange utaratibu wa kuwahoji.

Aliyewahi kuwa Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, alisema kama ingekuwa inawezekana, bunge lingevunjwa na wananchi wakarudi kuchagua wabunge wengine wa kubeba matatizo yao.

"Kama Katiba ingekuwa inaruhusu, tungeshauri bunge livunjwe na uchaguzi urudiwe kuchagua wengine wenye uchungu na wananchi wao. Lakini kwa sababu Katiba hairuhusu inabidi wananchi wahesabu tu kwamba wamepata hasara. Wajipange katika uchaguzi ujao kuwaondoa na kuwaweka wengine.

Heche alisema ni jambo la kusikitisha kuona wabunge ambao wameaminiwa na wananchi kushindwa kufahamu wajibu wao na badala yake kurushiana vijembe.

"Ukiangalia mpaka unasikitika, unajiuliza hili ni bunge la namna gani, kiukweli hili halijawahi kutokea. Mtaani huku wananchi wana matatizo kibao, watu walalia na ajira, kuna changamoto kwenye sekta mbalimbali, lakini hayo yote wabunge hawaoni, wanakazana kumjadili mtu," alisema Heche.

Kwa upande wake Mwanasheria mbobezi na aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Kijo Bisimba, alisema kuna haja ya kuwapa elimu wabunge kuhusu wajibu wao.

"Kinachoendelea kwa wabunge wetu ni cha kusikitisha, inaonyesha wabunge hawana uwezo wa kujenga hoja, hawajui wajibu wao au hawajui nini cha kufanya."

"Hapa kuna haja kubwa labda wapewe semina ili wafahamu wajibu wao kama wabunge. Lakini pia kuna haja hata Spika wa Bunge naye asimame katika nafasi yake kuliko kuwaacha waendelee hivyo wanavyofanya maana hii ni hatari."

"Hii ni hatari kwa sababu hawa ndio wanategemewa watunge sheria kwenye sekta zote, sasa kama hawana uwezo wa kujenga hoja, itakuwaje. Ndiyo maana baadhi ya watu wanafikia hata uamuzi wa kusema bora bunge livunjwe wakachaguliwe wengine, kwa kweli hata mimi nawaunga mkono."



Rais, Samia Suluhu Hassan akimuapisha Mkuu wa Itifaki katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Yusuph Tindi Mndolwa, kuwa Balozi katika hafla fupi iliyofanyika katika Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma **PICHA: IKULU.**

# Samia kulihutubia Bunge Alhamisi

**Na Gwamaka Alipipi,**

DODOMA

RAIS, Samia Suluhu Hassan, anatarajia kulihutubia Bunge pamoja na kuzungumza na Watanzania Alhamisi bungeni jijini Dodoma.

Rais Samia pamoja na mambo mengine, atatumia fursa hiyo kueleza mwelekeo wa serikali yake ya awamu ya sita kwa kuzungumzia mambo mbalimbali muhimu kwa Taifa

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alitoa taarifa hiyo jana bungeni baada ya kipindi cha maswali na majibu kumalizika na kueleza kuwa Rais Samia atalihutubia Bunge.

Kwenye taarifa hiyo, Spika Ndugai alisema: "Rais Samia Suluhu Hassan, atakuja hapa bungeni kwa ajili ya kulihutubia Bunge. Kwa hiyo atalihutubia Bunge na kuwahutubia Watanzania wote kupitia bunge kuanzia saa 10 jioni. Baada ya hotuba yake tutapata futari ya pamoja ambayo atakuwa ametuandalia yeye."

Spika Ndugai alisema futari hiyo itahusisha wabunge wote na watumishi wa Bunge na wageni waalikwa watakaokuwa wamejaa kwenye jukwaa maalum ya wageni (gallery) watakaotoka sehemu mbalimbali.

"Kama mnavyojua Rais akihutubia Bunge basi 'gallery' zetu zinakuwa zimejaa, maana tunaalika mabalozi, marais wastaafu na viongozi wa ngazi mbalimbali wanakuwapo hapa bungeni."

Spika Ndugai aliwataka wabunge wanaoomba kusafiri kujaribu kuweka sawa ratiba zako kwa kiwango ambacho siku hiyo jioni wanakuwapo jijini Dodoma.

Alisema: "Na kwa mbunge ambaye hayupo jijini Dodoma tufanye juhudi za kuhakikia anakuwapo Dodoma siku hiyo na kusikiliza hotuba hiyo muhimu kwa bunge na taifa."

Hiyo itakuwa ni mara ya kwanza kwake kulihutubia Bunge tangu alipoapishwa kuwa Rais Machi 19, mwaka huu baada ya kifo cha Rais wa tano, Hayati John Magufuli kilichotokea Machi 17, mwaka huu.

Rais Samia atatoa hotuba hiyo zikiwa zimebaki siku chache kwa chama chake (CCM) kikiwa kwenye hatua za maandalizi ya kufanya Mkutano Mkuu wa dharura Aprili 30, mwaka huu, kwa lengo la kumpa uenyekiti.

Tangu alipoapishwa kuwa Rais, Rais Samia kwenye hotuba zake amekuwa akisisitiza ukusanyaji wa mapato wenye haki pasipo kutumia mabavu, uwapo wa uhuru wa habari kwa kutoa agizo televisheni za mtandaoni zilizofungiwa kufunguliwa.

Mbali na hilo, Rais Samia kwenye hotuba zake amekuwa akiwataka Watanzania kujenga na kudumisha umoja wa kitaifa, kwa kupeana faraja na upendo.

Kadhalika, Rais Samia kwenye moja ya hotuba zake aliagiza kushughulikiwa kwa haraka kesi zilizopo na zisirundikwe, kesi zisizo na mashiko zisipelekwe mahakamani.

Baadhi ya mambo ambayo amekuwa akiombwa kuyatekeleza tangu aingie madarakani ni kufufuliwa kwa mchakato wa katiba mpya na makundi mbalimbali kuomba kukutana naye.

## HABARI KITAIFA

# Serikali kuwaondolea vikwazo wawekezaji

Na Julieth Mkireri, KIBAHA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka wawekezaji kuendelea kuiunga mkono serikali, huku akiahidi vikwazo vilivyokuwapo awali kuendelea kutatuliwa.

Majaliwa aliyasema hayo jana mjini Kibaha, mkoani Pwani, alipotembelea Kiwanda cha kuunganisha magari cha GFA Assemblers kilichopo eneo la Tamco Mailimoja.

Alisema moja ya shughuli zinazosimamiwa na ofisi yake ni uwekezaji, hivyo jukumu la serikali ni kuhakikisha mwekezaji hapati kikwazo na usimamizi kwa waliowekeza uko vizuri ili waweze kufikia malengo yao.

" Hayo ni maono ya waanzilishi wa awamu ya tano, awamu hii ya sita hatuna shaka malengo yalishawekwa utekelezaji unaendelea, tunatamani kuona viwanda vya namna hii ni vingi, waliokuwa wanadhani Watanzania hawawezi ni zana tu, utaalamu tunao tunatakiwa kuwadhihirishia," alisema.

Majaliwa alitoa wito kwa wafanyakazi kuendelea kuwa waaminifu, huku akiendelea kumsisitiza mkurugenzi wa kiwanda hicho kupanua wigo wa uwekezaji.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, alisema kiwanda hicho ni kati ya viwanda 1,438 vilivyopo katika mkoa huo.

Ndikilo alisema kiwanda hicho ni kati ya viwanda 1,100 vilivyojengwa katika kipindi cha miaka mitano kutoka viwanda 300 vilivyokuwapo awali.

Alisema uwapo wa ongezeko la viwanda katika mkoa huo umesababisha ongezeko la makusanyo ya mapato kutoka Sh. bilioni 65 mwaka 2015 na sasa kumfikia Sh. bilioni 147.

Mkuu huyo wa mkoa alieleza kuwa kipo kiwanda kingine cha kuunganisha magari ya abiria ambacho kinamilikiwa na Mtanzania Jonas Nyagawa ambacho kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kuunganisha mabasi 50 kwa mwaka.

Mkurugenzi wa Kiwanda hicho, Aljawad Karimal, alisema hadi kukamilika kinatarajia kugharimu Sh. bilion 12 kwa awamu mbili ambapo hadi sasa imetumia kiasi cha Sh. Bilioni nne.

Aliomba pia serikali kutoa zabuni ya kusambaza magari ya kubebea taka, magari ya majisafi, ya kubebea wagonjwa na magari ya jeshi ambayo yanaweza kuunganishwa katika kiwanda hicho na kufungua wigo wa masoko kwenye halmashauri.

# Rais ateua viongozi bodi, taasisi

Na Christina Mwakangale

RAIS Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa viongozi mbalimbali ikiwamo wenyeviti wa mabaraza, bodi na taasisi za serikali.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, rais amemteua Dk. Richard Masika kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT).

Alisema uteuzi huo umeanza Aprili, 16 mwaka huu, akichukua nafasi ya marehemu Prof. Apollinary Peleka.

Kadhalika, rais amemteua Prof. Joseph Msambichaka kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC), uteuzi ambao ulianza Aprili, 15 mwaka huu akichukua nafasi ya Prof. Manase Salema.

Pia, Revocatus Mushumbusi, ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) na kwamba uteuzi huo ulianza Aprili 16, akichukua nafasi iliyoachwa wazi na Dk. Ladislaus Nshubemuki aliyestaafu.

Vilevile, rais, amemteua Prof. John kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) baada ya kumaliza muda wa kipindi cha kwanza, uteuzi ambao ulianza Aprili 15, mwaka huu.

Kwenye uteuzi huo wamo pia, Dk. Mboni Ruzegea aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB), uteuzi wake ulianza Aprili 16, akichukua nafasi iliyoachwa wazi na Dk. Ali Mcharazo ambaye amestaafu.

Taarifa hiyo, ilisema rais, amemteua Prof. Esther Hellen Lugwisha, kuendelea kushika nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali baada ya kumaliza muda wa kipindi cha kwanza, uteuzi ulioanza Aprili 15, mwaka huu.

Aidha, amemteua Kapteni, Ernest Bupamba, kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) huku Prof. Makenya Maboko akiteuliwa kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) baada ya wote kumaliza muda wa vipindi vya awamu ya kwanza, uteuzi wao ukianza Aprili 15, mwaka huu.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

## TAARIFA KWA UMMA

### KUONGEZWA KWA MUDA WA KUWASILISHA TAARIFA ZA WANUFAIKA WA MWISHO (BENEFICIAL OWNERS)

Dar es Salaam, Aprili 08, 2021

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) unapenda kuwataarifu Wamiliki wa makampuni na umma kwa ujumla kwamba Waziri wa Viwanda na Biashara, kupitia Tangazo la Serikali Na. 189 la tarehe 12 Februari 2021 ameongeza muda wa miezi kumi na miwili (12) kuanzia tarehe 1 Januari, 2021 kwa ajili kuwasilisha taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) kwa kampuni zilizosajiliwa kabla ya tarehe 1 Julai, 2020.

Takwa hili la kuwasilisha taarifa tajwa ni matokeo ya marekebisho ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 yaliyofanyika kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 (Finance Act, 2020) kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners).

Aidha Kifungu cha 459A cha marekebisho hayo, ambacho kilizitaka Kampuni zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 kabla ya tarehe 1 Julai, 2020 kuwasilisha taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) ndani ya kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 1 Julai, 2020.

BRELA kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha Kanuni za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) zitakazoweka bayana utaratibu wa kukusanya na kuhifadhi taarifa hizi.

BRELA inawataka Wamiliki wa makampuni na umma kwa ujumla kutumia vizuri muda huu wa nyongeza kuwasilisha taarifa husika mapema na sio kusubiri muda wa mwisho ili kuepusha usumbufu wa namna yeyote unaoweza kujitokeza.

**Imetolewa na**
**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**

Jengo la Ushirka, Mtaa wa Lumumba, S.L.P. 9393, Dar Es Salaam, Simu: +255-22-2181344, 2180113, 2180141, 2212800,
Nukushi: +255-22-2180371, barua pepe: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz , Tovuti: www.brela.go.tz

# Marekani yasaidia vifaa mapambano ya corona

**Na Mwandshi wetu**

SERIKALI ya Marekani, kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), ilikabidhi vifaa vya UVIKO-19 kwa Wizara ya Afya ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ubalozi wa Marekani nchini, mradi wa USAID wa Mnyororo wa Ugavi wa Afya duniani hivi karibuni ulinunua vifaa vya upumuaji na usafi wa mazingira vyenye thamani ya Dola za Marekani 400,000 (sawa na Sh. milioni 927.6).

Ilieleza vifaa hivyo viliwasili mwezi uliopita kupitia Bandari ya Zanzibar na kusambazwa kwenye vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kupitia bohari kuu ya madawa.

"Shehena hiyo inajumuisha vifaa vya kupumulia kama vile vipimo vya mwenendo wa damu, mirija ya kupimia puani kwa watoto na watu wazima, barakoa na vifaa vya usafi wa mazingira kama vile dawa za mkoba za kunyunyizia, na mifuko ya kuwekea taka hatarishi," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Akizungumzia kuhusu utoaji wa vifaa tiba, Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Dk. Abdullah Ali, alisema: "Tunaamini katika uhusiano wa ushirikiano ambao unatoa huduma bora za afya kwa watu wote. "Shehena ya vifaa tiba vilivyopokelewa vitaziba mapengo yaliyopo katika kupunguza hofu inayohusishwa na tishio la UVIKO- 19 kwa suala la vifo, maradhi na kulazwa hospitalini."

Kwa kipindi cha mwaka mmoja sasa, Marekani imetoa Dola za Marekani milioni 16.4 kupunguza UVIKO-19 Tanzania.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Serikali ya Marekani inafurahi kushirikiana na Wizara ya Afya ya Zanzibar kutoa vifaa hivi muhimu, huku ikimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuunda kamati ya timu ya wataalam kumshauri kisayansi juu ya suala la corona.

**Ilieleza vifaa hivyo viliwasili mwezi uliopita kupitia Bandari ya Zanzibar na kusambazwa kwenye vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kupitia bohari kuu ya madawa.**

# PM amsimamisha kazi Mkurugenzi fedha DART

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amemsimamisha kazi Mkurugenzi wa Fedha wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Suzana Chaula, baada ya kutoridhishwa na utendaji wake.

Akizungumzia Mtendaji Mkuu wa wakala huo, Mhandisi Ronald Rwakatare, Waziri Mkuu amesema suala hilo atalikabidhi kwa mamlaka ya uteuzi.

Waziri Mkuu amechukua hatua hiyo jana wakati alipotembelea Kituo Kikuu cha DART-Gerezani na kuonesha kutoridhishwa na utendaji wa viongozi hao.

"Tangu Mtendaji Mkuu ameingia DART ana miaka mitano hakuna hata basi moja alilonunua, na anasema hana fedha kwani abiria hawasafiri? Si kila siku wanapigania kule Kimara na wote wanalipa unasemaje hakuna fedha ya kununulia magari."

Alisema tangu mradi huo ulipoanza mabasi yamekuwa yakipungua kutoka 140 hadi 85. "Watendaji wapo tu wamekaa ofisini wanapigwa na AC (viyoyozi) wananchi wanaumia. Hatuna sababu ya kumbakiza mtu kama hafanyi kazi".

Kadhalika Waziri Mkuu alisema wakala huo ulianzishwa na serikali kwa ajili ya kuondoa adha ya usafiri kwa wananchi, lakini viongozi hao wameshindwa kusimamia vizuri na kusababisha mradi huo kutoendelea vizuri.

Alisema mapato mengi ya serikali yamekuwa yakipotea kutokana na uendeshaji wa wakala huo. "Kwa nini ukatishaji wa tiketi haufanyiki kwa njia ya kielektroniki kwa asilimia 100? Tiketi zinauzwa kwa vifurushi."

"Haiwezekani watu wanafanya ujanja ujanja tu wakuja na tiketi zao za mfukoni halafu wakimaliza anauza za POS (Mashine ya Kielektroniki ya Kukusanyia Mapato) na wasimamizi wapo tu mkurugenzi wa fedha yupo tu ameshindwa kusimamia hili na lipo mikononi mwake."

"Kwa nini mnauza tiketi kwa vifurushi hamtumii mashine kukata tiketi. Mnaua wakala huu kwa sababu wauzaji wa tiketi wanakuja na tiketi zao na nyingine mnazileta nyinyi. Hamuwezi kusimamia mradi huu wa kimkakati."

Pia, Waziri Mkuu ametembelea karakana ya UDA ya Kurasini, Dar es Salaam na kushuhudia baadhi ya mabasi ya wakala huo yakiwa mabovu na alipouliza yanakabiliwa na changamoto gani Mhandisi Rwakatare alisema yana tatizo la mfumo wa gia (gearbox).

Hata hivyo, Waziri Mkuu alibaini kuwa magari hayo yanachangamoto nyingine na siyo gearbox pekee kwa sababu mengine yalikuwa yameondolewa baadhi ya vipuri, viti pamoja na matairi.

"...Unanidanganya gearbox ndiyo imeharibika wakati magari chakavu hivi yameharibika kabisa, kama gearbox ndio tatizo mbona kwenye magari mengine mmetoa hadi viti na matairi?

Wakati huo huo, Waziri Mkuu amemuagiza Meneja wa Forodha Bandari ya Dar es Salaam, Njaule Mdendu, kuhakikisha mizigo ya wateja katika bandari hiyo inatoka kwa wakati. Alitoa agizo hilo alipotembelea Kituo cha Forodha Bandari Kavu iliyopo Ubungo, mkoani Dar es Salaam.



Abiria wakitembea kwa tahadhari kutokana na matope katika stedi ya Kawe Manispaa ya Kinondoni jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mume mbaroni tuhuma kumuua mke kwa kumcharanga mapanga

**Na Ibrahim Yassin,** KYELA

MKAZI wa kitongoji cha Butiama, wilayani Kyela, Amini Sanga (36), anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kumuua mkewe Maria Mahenge (25) kwa kumcharanga mapanga kwa madai ya wivu wa mapenzi na yeye kujaribu kujiua kwa kujichoma kisu na kunywa sumu.

Tukio hilo limetokea juzi saa 2.30 usiku baada ya mwanamume huyo kudaiwa kwenda kwenye chumba cha mwanamke huyo (marehemu) ambaye inadaiwa alikuwa mke wake kabla ya kutengana.

Taarifa zinadai kuwa mwanamume huyo baada ya kuona mke huyo ameanza kupendeza alianza kumfuatilia kwenye chumba alichopanga kwa madai ya kwenda kusalimia watoto.

Mmoja wa jirani wa eneo hilo, Maria Mwabukusi, aliwambia mwandishi wa habari hizi kuwa mwanamke huyo alipoachana na mumewe aliamua kujipangia chumba na alipoanza kupendeza mumewe akaanza kuingiwa na wivu akidhani amepata mwanamume mwingine na kujifanya kwenda kuwasalimia watoto na kuamua kutekeleza mauaji hayo.

Alisema baada ya kufanya ukatili huo na yeye alijicharanga na kitu chenye ncha kali mwilini mwake kwa lengo la kujiua, lakini ilishindikana.

Alisema polisi baada ya kupata taarifa kutoka kwa viongozi wa kitongoji walifika na kumkamata.Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mjumbe wa Nyumba Kumi, Cheusi Maulidi, mauaji hayo yamefanyika katika eneo lake huku wakazi wakiwa hawatambuliki katika maeneo hayo kwa madai mwanamke alipanga katika mtaa huo bila kutoa taarifa.

Hata hivyo, alisema alipokea taarifa za ugomvi kutoka kwa majirani na baada ya kufika eneo la tukio alikuta mauaji tayari yamefanyika na kuchukua jukumu la kutoa taarifa polisi ambao walifika mapema.

Mwenyekiti wa kitongoji cha Butiama, Yohana Mwambungu, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo huku akidai kuwa ni la kwanza katika eneo hilo na kwamba marehemu ameacha watoto wawili aliozaa na mwanamume huyo aliyetekeleza mauaji hayo.

"Kuna uwezekano ikawa ni wivu wa kimapenzi kwa kuwa mwanamke huyo baada ya kuachana na mumewe alijipangia huku akijifanyia shughuli zake mwenyewe," alisema.

Naye Diwani wa Kata ya Mbugani, Ipyana Mwakila, (Msauth) alisema mtuhumiwa anashikiliwa na jeshi la polisi huku akiendelea na matibabu katika hospitali ya wilaya ya Kyela, chini ya ulinzi, akisubiri sheria ichukue mkondo wake.Mganga Mfawidhi wa hospitali ya Wilaya ya Kyela, Dk. Ray Salandi, alithibitisha kumpokea mtu huyo na kusema kuwa alipokelewa saa tatu usiku wa April 17, mwaka huu akiwa na jeraha kwenye mkono wa kushoto huku akiwa amekunywa dawa isiyofahamika akiwa na lengo la kujiua.

Alisema baada ya kupatiwa matibabu aliruhusiwa kutoka April 18, mwaka huu, chini ya ulinzi wa polisi akiwa anaendelea vizuri.

Kamanda wa Polisi mkoani Songwe, Urlich Matei, alisema mtuhumiwa alitenda tukio hilo la mauaji kwa kumchoma mkewe kwa kisu maeneo kifuani na shingoni na kumsababishia kifo huku na yeye akijaribu kujiua pasipo mafanikio.

Alisema jeshi la polisi mkoani Mbeya linalaani tukio hilo na kuwataka wananchi hasa wanandoa kuacha vitendo hivyo vya kuwaua wake zao na wao kujaribu kujiua kwa kuwa hilo si suluhisho la matatizo na pia aliwataka viongozi wa mitaa, vitongoji na vijiji kutoa elimu kwa wananchi ili waachane na vitendo hivyo.

## Wafanyiwa upasuaji huku moyo unadunda

**Na Frank Monyo**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), imewafanyia upasuaji wa kupandikiza mishipa ya damu na mishipa mikubwa ya kifua kwenye moyo wagonjwa 22 wakati moyo ukidunda.

JKCI iliendesha kambi hiyo maalum kwa kushirikiana na Daktari bingwa wa upasuaji wa moyo na mishipa ya damu, Subhash Sinha wa Hospitali ya MAX iliyopo New Delhi nchini India.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Mohamed Janabi, alisema kabla ya matibabu hayo JKCI kwa miaka mitano walikuwa wanapandikiza mishipa ya damu kwenye moyo kwa kuusimamisha kufanya kazi.

"Ngoja hili niliweke sawa, sisi tulikuwa tunafanya hizi operesheni kwa miaka mitano, tofauti kubwa na hii ni kwamba sisi tulivyokuwa tunafanya tulikuwa tunasimamisha moyo kabisa na kufanya upasuaji na baada ya hapo tunaushitua moyo na operesheni inakuwa imekwisha," alisema Dk. Janabi.

Alisema kuwa opereshani hiyo imegharimu jumla ya Sh. milioni 330 na kwamba kila moja imegharimu Sh. Milioni 15, na kama wagonjwa wangepelekwa nje ya nchi matibabu yangegharimu Sh. Milioni 990.

"Wagonjwa hawa kama tungewapeleka nje gharama yake ingekuwa mara tatu tuliyotumia hapa, hapo tungetumia kama milioni 960, hizi ni operesheni kubwa na zimekwenda vizuri, wagonjwa waliopandikizwa mishipa wakati moyo unapiga wagonjwa wote wapo salama na wanaendelea vizuri, lakini tumewapoteza wagonjwa watatu katika upasuaji wa mshipa mkubwa," alisema.

# Hati chafu kuwaadhibu watumishi halmashauri 53

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ummy Mwalimu, amesema watumishi wa halmashauri 53 zilizotajwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kupata hati chafu, watachukuliwa hatua stahiki za kisheria na kinidhamu.

Amesema TAMISEMI itafanya uchambuzi wa taaifa za halmashauri hizo, kubainisha sababu za matokeo hayo na kuchukua hatua hizo kwa watumishi watakaothibitika kuwa chanzo cha kutofanya vizuri kwa halmashauri zao.

Alitangaza hatua hiyo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa wizara yake kwa mwaka wa fedha 2021/22.

"Taarifa ya CAG kuhusu hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2019/20 imebainisha kwamba halmashauri 53 zimepata hati zenye shaka na halmashauri nane zimepata hati zisizoridhisha (Hati Chafu). Kufuatia matokeo hayo yasiyoridhisha," alisema Waziri Mwalimu na kuongeza:

"TAMISEMI itafanya uchambuzi wa taarifa za halmashauri zote zilizopata hati chafu na hati zenye shaka kubainisha sababu za matokeo hayo na kuchukua hatua stahiki za kisheria na kinidhamu kwa watumishi wote watakaothibitika kuwa chanzo cha kutofanya vizuri kwa halmashauri zao".

AFYA

Kuhusu malengo mahususi yaliyopangwa kutekelezwa na wizara yake kwa mwaka wa fedha 2021/22, Waziri Mwalimu alisema wanatarajia kujenga kujenga vituo vya afya vipya 121 kwa Sh. bilioni 60.50 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Alisema pia wanatarajia kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya 52 kwa gharama ya Sh. bilioni 15.60 vilivyoanza kujengwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa kutumia fedha za ndani.

Alisema pia serikali itaendeleza ujenzi wa hospitali za halmashauri 68 za awamu ya kwanza zilizoanza kujengwa mwaka wa fedha 2018/19, ikiwamo Hospitali ya Uhuru iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino iliyotengewa Sh. bilioni 55.70.

Alisema pia kutafanyika uendelezaji wa ujenzi wa hospitali 27 za awamu ya pili zilizoanza kujengwa mwaka wa fedha 2019/20 na hospitali nne za awamu ya kwanza, kwamba Sh.bilioni 11.40 fedha za ndani zimetengewa.

Alisema kutafanyika ukamilishaji wa maboma ya zahanati 763 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi katika majimbo yote ya uchaguzi, yatakayogharimu Sh.bilioni 38.15 ambapo kila zahanati imetengewa Sh.milioni 50," alisema Waziri Mwalimu.

Alisema pia kutaanzwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa shule 10 kati ya 26 za sekondari za wasichana za bweni kwa masomo ya sayansi (shule moja kwa kila mkoa) ambayo katika awamu ya kwanza itajengwa miundombinu ya kidato cha tano na sita.

Alisema shule hizo zitakapokamilika zitakuwa na kidato cha kwanza hadi cha sita, kuwa na uwezo wa kupokea wanafunzi kati ya 1,000 hadi 1,200 kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP), kwamba Sh. bilioni 40 zimetengwa.

Alisema pia kutajengwa shule mpya 300 za sekondari za kutwa kwenye kata ambazo hazina shule za sekondari kwa gharama ya Sh. milioni 650 hadi 700 kwa kila shule kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari.

Kadhalika, alisema kutafanyika ukamilishaji wa maboma ya vyumba 3,268 kwa madarasa ya shule za msingi kwa gharama ya Sh. bilioni 40.85, Kuhakikisha upatikanaji wa madawati ya shule za msingi 710,000 ili kukabiliana na upungufu wa madawati 1,048,561.

# Spika ataka wabunge CCM kufanya kikao badala kusemana bungeni

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amekishauri Chama Cha Mapinduzi (CCM), kuitisha kikao cha wabunge (party caucus) endapo wanadhani kuna makundi ama mgawanyo wa wabunge ndani yao.

Amesema kama kuna mtu analengo binafsi ni vyema kukaitishwa kikao na kuwekana sawa kuliko kusemana ndani ya mhimili wa bunge ama hadharani.

Spika Ndugai alilazimika kutoa kauli hiyo baada ya Mbunge wa Viti Maalum, Lucy Mayenga, kueleza bungeni kwamba kumekuwapo na tabia ya baadhi ya wabunge kupingana wenyewe, pamoja na kukosa umoja na mshikamano.

Kutokana na kutoa hoja hiyo, Spika Ndugai alisema: "Katibu wa caucus tuitishe vikao vya mara kwa mara kama mnaamini kuna makundi kati yenu ili mthibitishe na siyo hapa (bungeni) mahali ambapo mnatuhumiana na kujibizana."

Aliongeza: " Mkifanya hapa (bungeni) mnatupa wakati mgumu, mi sijui makundi kwa sababu Bunge hili ni jipya, Rweikiza itisha kikao, siasa ni makundi ili mradi yasilete sumu ya kutufanya tusisonge mbele, mimi sioni kama tunayumba lakini kama kuna makundi tuzungumze huko kwenye cocus (kikao cha chama) siyo hapa."

Wakati akichangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2021/22, Mbunge Mayenga alisema: "Nampongeza Rais Samia Suluhu Hassan, sina shaka naye najua ni mfuatiliaji, ni mtu wa vitendo na ninamfahamu kama wabunge, lakini maendeleo yoyote katika TAMISEMI hayataweza kufikiwa kama hakutakuwa na umoja kuanzia juu hadi chini kwenye ngazi za mikoa hadi kijijini."

"Lipo jambo ambalo Rais Samia amelisema jana kwa nafsi yangu siwezi kuacha likapita kimya kimya, alisema humu ndani mwenendo wetu lazima tuangalie, ile kauli unaweza kuiona kama ni ndogo vile, lakini vipo humu ndani vitu ambavyo vinatusababishia kukosa umoja na mshikamano, ninafahamu kwamba wapo watu tena ni wengi ambao mtu akipinga wao wanapinga kutoka moyoni na mtu akiunga bila kuangalia vyama kuna mtu pia anapinga," alisema Mayenga.

# Waziri aja na mwaronaini sekta ya kilimo

**Na Mwandsihi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amesema wizara yake imejipanga kuhakikisha wakulima wanapata mbolea bora na kwa wakati sambamba na mikakati ya kufanya tafiti za mbegu bora pamoja na upimaji wa afya ya udongo ili kuongeza tija kwenye kilimo.

Akizungumza na waandishi baada ya kikao cha kazi cha Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA), Prof. Mkenda alisema ili kilimo kiwe na tija, lazima kuweka mipango ambayo itaongeza uzalishaji ikiwamo upatikanaji wa mbolea bora, huku akipinga mapendekezo ya ongezeko la bei elekezi.

"Kama wizara hatukubaliani na mapendekezo ya ongezeko la bei elekezi kwa kuwa mipango na mikakati yetu ni kuongeza uzalishaji. Tuna jukumu la kumwondolea mkulima changamoto mbalimbali zikiwamo upatikanaji wa mbegu bora, upimaji wa afya ya udongo, gharama nafuu ya pembejeo pamoja na matumizi ya mbolea bora," alisema.

Prof. Mkenda ameitaka bodi hiyo kuongeza ufanisi kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti ya Kilimo (TARI) ili kuwezesha utoaji wa elimu ya upimaji wa afya ya udongo na kupendekeza matumizi stahiki ya mbolea.


## NOTISI YA MNADA WA HADHARA

WELLCASH DEBT COLLECTORS,Kwa idhini tuliyopewa na CRDB BANK PLC, MAKAO MAKUU,DAR ES SALAAM,tutauza kwa Mnada wa hadhara dhamana za wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali chini,endapo watashindwa kulipa madeni wanayodaiwa ndani ya muda wa siku kumi na nne(14) kuanzia tarehe ya tangazo hili..Mnada utafanyika mahali zilipo dhamana hizo kama tarehe zilivyoonyeshwa kwenye jedwali kuanzia saa 2:30 Asubuhi.

| S/N | TAARIFA ZA DHAMANA | MAELEZO ZAIDI/ENEO ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | Nyumba yenye Hati Namba 13874 MTW,iliyo kwa jina la SHAFII ISSA CHINOWA | Kiwanja Na. 409, Kitalu "KK" Mdenga,Mtwara | 7/5/21 |
| 2 | Nyumba yenye hati Namba DSMT1000755 Usajili Namba. DSMS0020266 iliyo kwa jina la ALLY RASHIDI MODU | Kiwanja Na.P.3098 Mbezi Luis,wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam | 7/5/21 |
| 3 | Nyumba yenye dhamana ya makubaliano iliyo kwa jina la RITUNGU TOURS & SAFARI LTD | Stendi ya Dodoma, Wilaya ya Mvomero, Dodoma | 7/5/21 |
| 4 | Gari lenye usajili T247DQZ lililo kwa jina la SEREKA MAXIMILLIAN ALOYS | BMW-Saloon(Closed Top) | 8/5/21 |
| 5 | Gari lenye usajili T711AMW lililo kwa jina la RITUNGU TOURS & SAFARI LTD | TOYOTA-Land cruiser (Hardtop) | 8/5/21 |
| 6 | Gari lenye usajili T483ADV lililo kwa jina la RITUNGU TOURS & SAFARI LTD | Land Rover Discovery (station wagon) | 8/5/21 |
| 7 | Gari lenye usajili T989ALD lililo kwa jina la RITUNGU TOURS & SAFARI LTD | Mitsubishh-Pajero(station wagon) | 8/5/21 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada na salio la 75% litalipwa ndani ya siku kumi na nne(14).
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio ndani ya siku 14, atakuwa amepoteza haki yake ya malipo ya 25% na dhamana itauzwa upya.
3. Gharama zote kuhusu kubadilisha jina na umiliki wa dhamana zitakuwa juu ya mnunuzi.
4. Baada ya kukamilisha maliyo yote ni jukumu la mnunuzi kumuhamisha mkazi/wakazi waliopo ndani ya nyumba husika

**Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi:**
**Wellcash Debt Collectors Limited**
**Dar Free Market Mall, first floor, office No.7**
**Dar es Salaam**
**+255 758 182 094, +255 768 000 307**
**arnold@wellcashdc.com**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tuangalie mafuta hayo yana viwango?

**SUALA** la mafuta ya kula kuwa changamoto kila wakati limeanza kuwa kama jambo la mazoea. Kama ambavyo sukari nayo inafika kipindi ikaondoka sokoni kwa maelezo kuwa wazalishaji wanasafisha vikaango, vivyo hivyo mafuta nayo yanapotea.

Kuna maelezo kuwa miwa ikishakamuliwa 'juisi' yake inapitishwa katika mitambo ya kuikausha ili iwe kama 'mchanga' ambayo ndiyo sukari na eneo inapokaushiwa huitwa kikaango.

Changamoto ya sukari kuadimika kama yalivyo sasa mafuta imekuwa ni suala la mara kwa mara na kinachotokea kwenye upungufu huo ni maduka kuongeza bei na sasa ndicho kinachotokea kwenye mafuta.

Hata hivyo, kinachotusukuma leo ni kuzungumzia mafuta. Kwa muda mrefu suala la mafuta halijaeleweka kwa vile sokoni kuna aina ya mafuta ya kula 'isiyoeleweka' au ya viwango duni.

Mafuta hayo ndiyo yanayotumiwa na wapishi wa aina mbalimbali iwe migahawani, mama na babalishe na kukaanga vitafunio mbalimbali kama mihogo, chips , ndizi na vyakula vingine vingi.

Yapo kwenye ndoo kubwa na ndogo na hata madumu ambayo wateja hupimiwa kwenye vipimo vidogo au lita moja wanaponunua rejareja lakini ukiyaangalia ni kama hayana viwango. Yanaelekea kana kwamba hayayeyuki. Yana masimbi Tena yameganda.

Haya ndiyo mafuta yanayotumiwa karibu kila mahali kukaanga chapatti na vitafunwa mbalimbali na ndiyo yanayotumika kupikia vyakula kwenye migahawa na sehemu kubwa mijini na vijijini.

Ukifuatilia unakuta kuwa hayayeyuki kikamilifu na pengine hayana kiwango yakilinganishwa na mengine yanayoelezwa kuwa yamechunjwa mara kadhaa na kemikali ambazo pengine zina madhara kwa binadamu.

Mafuta yanayouzwa ghali ni yale ambayo yamechujwa na kusafishwa yakawa meupe na ndiyo ambayo huuzwa ghali zaidi na ndiyo yaliyoelezwa kuwa yameadimika.

Mafuta hayo tunafikiri wakati umefika wa kuyachunguza, tukishauri Shirika la Viwango pamoja na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba kutoa maelezo kuhusu ubora na viwango vyake kwa afya ya walaji.

Mafuta hayo yanauzwa kwa wingi kwenye chupa za plastiki yakijazwa kwenye chupa hizo zinazookotwa mitaani baada ya watu kuzitupa wakishamaliza kunywa maji.

Uuuzaji mafuta hayo yaliyojaa sokoni, madukani, mnadani na kwenye maeneo ya biashara za vyakula, unatia mashaka. Na hofu yetu ni kwamba huenda hayako salama kiafya kutokana na ukweli kuwa yanaganda, yana masimbi na rangi si angavu.


Licha ya maelezo kuwa kuna shehena ya mafuta ya meli iliyotoa nchini, bei za mafuta hasa ya viwango vya juu au yaliyochunjwa 'double refined' yanayotumiwa na wachache bei zake zimeendelea kupaa. Lita moja ikiuzwa Sh. 8,000 kwa jumla na takribani 10,000 kwa rejareja.

Ukweli ni kwamba mafuta yanayotumiwa mitaani kukaanga vyakula kuanzia samaki hadi vitumbua yanaibua maswali mengi na mara nyingi huwa hayaadimiki, wala bei zake hazibadiliki mara kwa mara.

Tunapendekeza mafuta hayo kuchunguzwa kwa sababu si wafanyabiashara wote wanaotoa taarifa za ukweli huenda wapo wadanganyifu na mara nyingi wanakwepa kuuza bidhaa hiyo kwa utaratibu unaofahamika na badala yake huwapa wamachinga wawasaidie kuuza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Elimu, ushiriki wadau tiba vita mimba utotoni

**MIMBA** kwa wanafunzi zinatajwa kuchangiwa na mengi, miongoni mwake ikiwa ni kutembea umbali mrefu kutoka nyumbani kwenda shuleni na kurudi jioni. Wakiwa njiani mabinti wanakumbana na vishawishi kadhaa.

Kinachowashawishi ni pamoja na lifti kutoka kwa madereva wa bodaboda, ili kuwawahisha shule au nyumbani, lakini lengo la waendesha pikipiki ni kuwa na uhusiano ya kingono.

Kwa wanafunzi ambao ni wepesi kushawishika kwa lifti , hujikuta katika wakati mgumu, kwa kukatisha masomo kutokana na kupata ujauzito na hivyo kujiharibia maisha na mlengo ya baadaye.

Mimba hizo kwa namna moja au nyingine, zinachangia kukwamisha hata Malengo ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu (SDGs), hasa lengo namba 4 linalohusu elimu kwa wote pamoja na usawa wa kijinsia.

Zipo jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali pamoja na wadau wa elimu kwa ajili ya kumaliza tatizo hilo la mimba shuleni, hasa kwa wanafunzi wanaotembea umbali mrefu kufuata elimu.

Miongoni mwa juhudi hizo za serikali ni ujenzi wa mabweni na pia kuagiza wanafunzi kusoma katika shule, ambazo ziko karibu na maeneo wanayoishi, ili kuwaepusha na vishawishi njiani.

Lakini , pia katika mwendelezo huo wa kukabiliana na mimba, Rais Samia Suluhu Hassan, anaiagiza Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kukamilisha ujenzi wa shule za wasichana 26 nchi nzima ifikapo 2025.

Mradi huo unalenga kuboresha mazingira ya watoto wa kike katika kupata haki ya elimu ili kuleta uwiano sawa wa haki ya kupata masomo kama ilivyo kwa wanaume.

Ni imani ya wengi shule hizo zikiwa na mabweni, zinaweza kuepusha wanafunzi husika, kuepuka vishawishi ambavyo baadhi yao hukutana navyo njiani na kusababisha wakatishe masomo kwa kupata ujauzito.

Pamoja na hayo, bado kuna njia nyingi ambazo ni vyema zikaendelea kutumika kwa ajili ya kupunguza tatizo hilo, ikiwamo wazazi na walezi kuimarisha malezi bora kwa watoto wao.

Katika hilo na wazazi na walezi wana jukumu la kuhakikisha wanafuatilia kwa karibu mienendo ya watoto wao, kwa kuwa hatua hiyo inaweza kusaidia kupunguza ukubwa wa tatizo.

Aidha, ni vizuri zaidi wazazi na walezi katika malezi yao, wasiwaache watoto wakawa na uhuru uliopitiliza bila kufanya ufuatiliaji, ambao unaweza kuchangia kuwangiza katika matatizo.

Vilevile elimu ya afya ya uzazi nayo ina nafasi kubwa katika malezi, kwa kuwa inasaidia kuwafanya wajitambue, ili hata wanapokutana na vishawishi vikiwamo vya lifti, wanakuwa na ujasiri wa kuvikwepa.

Suala la kuwapo kwa klabu za wanafunzi shuleni nalo lina umuhimu, kwa kuwa wanapata nafasi ya kukutana na kujadili mambo mbalimbali na mbinu ya kujiweka pembeni na mambo yanayoweza kuwaharibia malengo yao.

Klabu za wanafunzi zina mchango kwao, kwa kuwa kupitia elimu wanayopata inaweza pia kubadilisha fikra na kuwakomboa kutoka katika mazingira ambayo ni hatari kwa maendeleo yao ya kielimu.

Njia hizo na nyingine nyingi, zinaweza kuwa na mchango mkubwa katika vita dhidi ya mimba kwa wanafunzi, iwapo kila mmoja wetu atashiriki kikamilifu kutoa mchango wake wa kupiga vita tatizo hilo.

Ikumbukwe, lengo la mradi wa ujenzi wa shule 26 alizosema rais, ni kuboresha mazingira ya watoto wa kike nchini, kupata haki ya elimu ili kuleta uwiano sawa wa haki ya kupata masomo kwa watoto wa kike na kiume.

Hivyo, ni muhimu jamii kushiriki katika vita hiyo yenye lengo la kumsaidia mtoto wa kike ili naye aweze kufikia malengo yake katika elimu badala kukwamishwa na mambo ambayo wakati mwingine anaweza kunusuriwa.

Kushirikiana na wadau wa masuala ya kijinsia na afya kunaweza kuleta mafanikio kwenye kukomesha ukatili huo kwa wanafunzi ambao umekuwa ukiripotiwa kuwapo nchi kila mwaka.

Wadau wa masuala ya jinsia wana msaada mkubwa kwa wanafunzi wa kike wanaoishi katika mazingira hatarishi kwa kuwa ushauri wao unaweza kusaidia kufanya wahusika kutoa taarifa katika vyombo mbalimbali ikiwamo polisi na taasisi nyingine wanapokutana na vishawishi.

HABARI KITAIFA

# Ufaransa yatoa bil. 1.7/- kujengea uwezo wasichana

**Na Salome Kitomari**

UBALOZI wa Ufaransa nchini, unatarajia kutoa Dola za Marekani 720,000 (sawa na Sh. Bilioni 1.7) kwa ajili ya mradi wa kuwajengea uwezo wasichana kupitia kilimo hai katika mikoa ya Dodoma (Kogwa), Tabora (Nzega) na Zanzibar.

Akizungumza wakati wa kutambulisha mradi huo jana jijini Dar es Salaam, Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, alisema wanaamini katika kuwawezesha wanawake na kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa. Mashirika yasiyo ya kiserikali yatakayoshiriki utekelezaji wa mradi huo ni FCS Trust Limited, Msichana Initiative, Practical Permaculture Institute of Zanzibar na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT).

Alisema mradi huo utawafikia vijana 2,000, ikiwa ni asilimia 90 wasichana na asilimia 10 wavulana, ni mwendelezo wa mradi wa kilimo hai kwa wakulima wadogo uliotekelezwa mwaka 2019/2020 kwa gharama ya zaidi ya Dola milioni moja.

"Ufaransa inajivunia kuisaidia Tanzania katika mabadiliko ya kilimo cha kisasa, kwa kuzingatia kilimo endelevu kwa mipango ya maendeleo ya muda mrefu," alisema.

Kwa mujibu wa balozi huyo, mradi huo wa miaka miwili 2021 hadi 2021 watasaidia ubunifu na kukabili mabadiliko ya hali ya hewa.

Balozi Clavier alisema Ufaransa iliona matokeo ya uwezeshwaji kiuchumi kwa wanawake kupitia miradi yake ya awali ya kilimo hai, mafunzo kiasi cha kuibua wajasiriamali wadogo wa kilimo hicho.

Alisema kwa miaka ya hivi karibuni Tanzania imejionea upepo mkali, mvua nyingi, dhoruba na kuongezeka kwa joto, na kwamba kama hatua madhubuti hazitachukuliwa joto litaongezeka kwa nyuzi joto tatu hadi nne, na kwamba mwaka jana nchi ilishika nafasi ya tano duniani kwa kupoteza bionuwai.

Mkurugenzi wa Shirila la Wasichana Initiative, Rebeca Gyumi, alisema kwa muda mrefu wanawafikia wasichana kwenye masuala ya haki, usawa na kuripoti ukatili wanaopitia katika maisha yao ikiwamo ndoa za utotoni.

"Mradi huu ni muhimu sana unaenda kuwekeza kwenye baadhi ya matokeo tuliyoyaona kwenye ripoti za tathimini, wasichana wengi wanashindwa kuripoti ukatili kutokana na kukosa misingi na uwezo wa kiuchumi, mradi huu utaunganisha masuala ya usawa wa kijinsia, vita dhidi ya ukatili wa kijinsia na uwezeshaji kiuchumi kwa wasichana," alifafanua.

Naye, Mkurugenzi wa Shirika la Kilimo Endelevu (SAT), Janet Maro, alisema wamekuwa wakifanya shughuli za kilimo hai kwa zaidi ya miaka 10 na wameufikia mtandao wa wakulima 20,000 wa mikoa ya Morogoro na Dodoma.

Naye, Ofisa Mtendaji Mkuu wa FCS Trust Fund na Meneja Uendeshaji, Ikram Ramadhani Soraga wa Shirika la Practical Permaculture Institute of Zanzibar, walisema mradi huo kwa pamoja watawasaidia wasichana kujikita katika kilimo hai ili kupata lishe bora pamoja na usalama wa chakula.

# NMB yazindua bima simu za mkononi

**Na Beatrice Moses**

BENKI ya NMB kwa kushirikiana Kampuni ya Reliance Insurance, wamezindua huduma mpya ya bima, inayolenga kulipia gharama za matengenezo ya simu za mkononi za wateja wao wanaotumia huduma ya NMB Mkononi pale zinapoharibika.

Huduma hiyo iliyo chini ya mwamvuli wa BancAsuarance, inatambulika kama Muamala Wako, Bima Yako, ambako simu yenye NMB Mkononi, itakayotumia huduma hiyo angalau mara moja kwa mwezi, italipiwa gharama za matengenezo isiyozidi Sh. 500,000.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi, alisema Muamala Wako, Bima Yako ni huduma inayoenda kufaidisha zaidi ya wateja milioni 3 wanaotumia huduma ya NMB Mkononi kote nchini.

Aliongeza kuwa ubunifu wa kihuduma ni kipaumbele cha benki yake na kwamba wanaamini wateja wao wataifurahia sana bima hiyo na kwamba kutokana na kuongezeka kwa watumiaji wa simu za mkononi, wameona umuhimu wa kugusa mahitaji ya kila mteja.

Mkurugenzi Mtendaji (CEO) wa Reliance Insuarance, Ravi Shankar, aliliita tukio hilo la uzinduzi huo kuwa ni la kihistoria, huku akiwahakikisha wateja wa NMB Mkononi huduma bora na za haraka za malipo ya bima za matengenezo ya simu zao.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA), Emily Kiria, alizipongeza NMB na Reliance Insuarance kwa huduma hiyo, aliyosema inaunga mkono jitihada za Serikali kupitia mamlaka yake ya kuongeza uelewa na matumizi ya bima miongoni mwa Watanzania.




# Asasi zajadili sheria, miongozo

**Na Mary Geofrey**

ASASI za kiraia zimekutana kujadili matakwa ya sheria na miongozo inayosimamia na kuratibu sekta ya asasi hizo nchini, baada ya sheria hizo kufanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Mkutano huo ulioandaliwa na Foundation for Civil Society (FCS) kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Mtandao wa Mashirika yasiyo ya Serikali (TANGO) na Shirika la Equality for Growth (EfG) uliwakutanisha wadau hao kwa njia ya mtandao wa zoom.

Akizungumza kuhusu mkutano huo wa siku mbili, Meneja Idara ya Kujenga Uwezo wa FCS, Edna Chilimo, alisema lengo la kuwakutanisha wadau hao pamoja ni kutoa elimu juu ya utekelezaji wa sheria hizo, kuzipitia ili kuona namna ambavyo zitatekelezwa pamoja na kutoa fursa kwa wadau hao kutoa maoni yao.

"Kuna changamoto kubwa katika uelewa na tafsiri ya sheria hizo, wapo wengine walikuwa hawazielewi na wengine walikuwa na tafsiri potofu, wengine walihamaki hivyo FCS kama mwezeshaji baada ya kugundua tatizo tukashirikiana na wadau wengine ambao ni Mashirika ya kimtandao ambayo ni NaCoNGO, TANGO na EFG kutengeneza programu ya kuwawezesha asasi za kiraia kuzielewa vizuri," alisema Edna.

Alifafanua zaidi kuwa, wadau hao walielezwa tafsiri sahihi ili waweze kuzifuata na kuzifanyia kazi katika kutekeleza miradi yao kwa weledi katika kuwafikia wananchi.

Alisema mkutano huo ulizikutanisha asasi za kiraia zaidi ya 300 na mada mbalimbali zilitolewa na baadhi ya wataalamu kutoka katika Ofisi ya Usajili wa Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) Usajili wa Jumuiya za Kijamii, na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA).

Aidha, alisema katika programu hiyo licha ya kutoa elimu ya kuwajengea uwezo wa uelewa wa sheria hizo pia walilenga kutoa msaada kwa yale mashirika yaliyokuwa yanahitaji msaada wa kitaalamu katika kufikia malengo yao.

Kadhalika alisema FCS inajipanga kuandaa mkutano mkubwa zaidi kwa kushirikisha wadau wengi zaidi ili kuendelea kutoa uelewa juu ya sheria hizo.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Bilinith Mahenge, akitoa hotuba yake ya kufungua mafuzo ya siku mbili kuhusu huduma zinazotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa wakazi wa Dodoma katika ukumbi wa mikutano uliopo makao makuu ya Jeshi la Zimamoto, Jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kanisa Anglikana Nyasa lapata askofu

**Na Richard Makore,** MWANZA

KANISA la Anglikana Dayosisi ya Victoria Nyanza, jijini Mwanza, linatarajia kumsimika askofu mteule wa dayosisi hiyo, Zephania Ntuza.

Ntuza anatarajiwa kuwa askofu wa tano wa kanisa hilo katika dayosisi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kaimu Katibu wa Dayosisi ya Victoria Nyanza, jijini Mwanza, Mchungaji Canon Willison Mafumbi, alisema askofu huyo atasimikwa Mei 16, mwaka huu.

Alisema sherehe za kumsimika kiongozi huyo, zitahudhuriwa na maaskofu wote wa kanisa la Anglikana nchini.

Askofu huyo alichaguliwa kwa mujibu wa katiba ya kanisa hilo, Aprili 15, mwaka huu.

Akizungumzia sherehe hizo, Mchungaji Canon Shadrack Thobias wa Dayoyo ya Victoria Nyanza, alisema wanahudumia waumini wapatao 600,000 katika mikoa mitatu ya Geita, Simiyu na Mwanza.

Alisema dayosisi hiyo imekaa bila askofu tangu mwaka 2017 baada ya aliyekuwapo kustaafu utumishi huo.

## Madiwani walalamikia kituo cha afya

**Na Happy Severine,** BARIADI.

MADIWANI wa Halmashauri ya Bariadi mkoani Simiyu, wamekilalamikia kituo cha afya cha Muungano kwa utoaji wa huduma mbovu za afya.

Kituo hicho kinacholalamikiwa ni tegemeo kwa wakazi wa mji huo kwa ajili ya kupata huduma, lakini kwa sasa kimegeuka na kuwa mwiba kwa wananchi hao.

Wakizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Bariadi, mwishoni mwa wiki iliyopita, walimtaka Mkurugenzi na Idara ya Afya wa halmashauri, kutatua kero hiyo ili wananchi hao waweze kupatiwa huduma stahiki.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, David Masanja, alisema kituo hicho pia hakitoi huduma nyakati za usiku hali inayosababisha usumbufu kwa wananchi.

"Kituo hicho kinakuwa wazi nyakati za usiku, lakini hakuna huduma zinazotolewa wakati huo wala mganga anayekuwa zamu kutoa huduma... tunakuomba Mkurugenzi ufuatilie suala hili, wananchi wanalalamikia utoaji wa huduma kituoni hapo," alisema mwenyekiti huyo.

## Standard Chartered yaanza kuhamasisha mfumo wa kidigitali

**Na Enock Charles**

BENKI ya Standard Chartered jana imezindua shindano linalojulikana kama 'Bank more score more'katika mkakati wake wa kuingia katika mfumo wa matumizi ya benki kidijitali.

Kqdhqalika, imewaomba wananchi kuingia katika mfumo huo wa kisasa ili kukwepa hatari mbalimbali kama wizi na magonjwa kama Corona ambazo huweza kujitokeza katika mfumo wa kizamani.

Akizungumza na waandishi wa habari ,Jijini Dar es Salaam jana ,Mkuu wa Kitengo cha wateja binafsi wa benki hiyo Ajmair Riaz alisema lengo la shindano hilo ni kuwafanya wateja wao kufanya miamala ya kibenki kidijitali na kuondokana na mifumo ya kizamani katika kutunza na kutumia fedha zao.

"Katika mwaka huu tunakumbuka kuwa ni miaka miwili tangu tuanzishe benki ya kidijitali hapa Tanzania kwa hiyo mwezi huu tunaadhimisha miaka miwili"-alisema Riaz

Alisema kwa mwaka huu pekee benki hiyo imefikisha idadi ya akaunti laki moja na kuweza kuongeza idadi ya wateja wake kwa zaidi ya asilimia 700 ambapo ameeleza kuwa kabla ya kuzindua benki hiyo kidijitali miaka miwili iliyopita ilikuwa na wateja wanao tumia benki kidijitali 20,000 pekee na hivyo kuwapongeza watanzania kuitikia wito huo.

Shindano hilo linatarajiwa kupata washindi 40 kila wiki ambao watashinda baada ya ama kufungua akaunti, kuchukua mkopo au kutumia huduma zingine za benki hiyo ambapo mteja atapata pointi zitakazomuwezesha kushinda.

HABARI KITAIFA

## Wamiliki 220 majengo vyakula, vipodozi wasajiliwa

**Na Mwandishi Wetu,** UYUI

WAFANYABIASHARA wanaomiliki majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi wapatao 220 wa baadhi ya kata za wilaya za Sikonge na Uyui, mkoani Tabora, wamesajili na kupata vibali kwa ajili ya kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa sheria.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki wilayani hapa na Ofisa Uthibiti Ubora wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) Dodoma, Zena Mushi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ukaguzi na usajili wa majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi lililofanyika kwenye baadhi ya kata za wilaya hizo mbili.

Kwa mujibu wa Mushi, ukaguzi na usajili wa majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi katika wilaya hizo mbili ulianza Machi 29, mwaka huu na kuhitimishwa juzi wilayani Uyui.

Mushi alisema wamehitimisha kazi hiyo kwa awamu hiyo ya kwanza Wilaya ya Uyui kwa kufikia Kata mbili za Roya na Tura, ambapo walifikia wafanyabiashara 100 na wote wamepata vibali.

Alisema mwitikio wa wananchi kusajili majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi katika wilaya hizo umekuwa mkubwa na kwamba hicho ni kielelezo kuwa wafanyabiashara sasa wanataka kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi.

## Viongozi wa serikali awamu ya 6 waombewa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

VIONGOZI wa dini wametakiwa kutopingana na serikali badala yake wajikite kuhubiri amani na kuwaombea viongozi waliopo madarakani.

Wito huo ulitolewa katika ibada ya kushukuru Mungu kulipitisha Taifa katika uongozi wa awamu ya tano na kuingia awamu ya sita kwa amani.

Katika ibada hiyo iliyofanyika kwenye Kanisa la PMC Mailimoja na kuongozwa na Askofu Gervase Masanja wachungaji waliombea Taifa liendelee kudumu kwenye amani.

Wachungaji walioshiriki katika ibada hiyo walisema kubadilishana uongozi katika nchi nyingine ingekuwapo misuguano, lakini kwa Tanzania, Serikali ya awamu ya sita imeendelea kuongoza kwa amani na utulivu, jambo ambalo ni la kumshukuru Mungu kwa hali iliyopo.

# Kigogo CCM anayedaiwa kutishia maisha afunguka

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Songwe, Henerico Mkola, ambaye anatuhumiwa kumtishia maisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Hanji Godigodi, amefunguka na kusema asingeweza kufanya hivyo halafu vyombo vya ulinzi na usalama visikumchukulie hatua hadi sasa.

**Sikumtishia, kama ningemtishia mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa halafu niachwe nisichukuliwe hatua.**

Mwenyekiti huyo anadaiwa kumtishia mkurugenzi huyo baada ya kukataliwa kulipwa Sh. milioni 12 anazodai kusambaza vifaa vya ujenzi nondo na saruji zabuni ambayo inadaiwa ni hewa na tukio hilo kuripotiwa kituo cha polisi Vwawa na kufunguliwa RB kwa ajili ya upelelezi namba MBZ/IR/200/2021.

Mwenyekiti huyo amesema hafahamu kama kampuni zake za biashara zinaidai halmashauri hiyo kiasi cha Sh. milioni 12 kutokana na kusambaza vifaa hivyo.

"Sikumtishia, kama ningemtishia mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa halafu niachwe nisichukuliwe hatua," alisema Mkola wakati akizungumza na gazeti hili.

Alipoulizwa kama alisambaza vifaa hivyo kwa halmashauri na kudai alipwe Sh. milioni 12, alisema hawezi kufahamu kwa sababu ana watu ambao wanaendesha kampuni zake, hivyo wao ndo wanaweza kujua kama wanadai au la.

"Anayedai fedha halmashauri siyo Mwenyekiti wa chama bali mkurugenzi wa kampuni, kamuulizeni kama ana documents (nyaraka) atawaonyesha, unajua kuna uchaguzi ndani ya chama, kwa hiyo mahasimu wangu wa kisiasa wanajaribu kunichafua," alisema.

Mkola alisema kampuni zake tangu mwaka 1987 zimekuwa zikifanya biashara na halmashauri na anayehusika ni Rahabu Mkola ambaye ndiye mkurugenzi.

Alipoulizwa je, sheria inamruhusu kama kiongozi kuingia zabuni au kufanya biashara na halmashauri, alisema yeye ni mwenyekiti wa chama, kazi ambayo anaifanya kwa kujitolea halipwi mshahara.

Awali gazeti hili liliporipotiwa kwa mara ya kwanza, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, alipoulizwa alithibitisha suala hili liliripotiwa katika kituo cha polisi lakini lilishughulikiwa kiutawala.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbozi, Hanji Godigodi, alipoulizwa alikiri kutishiwa maisha na kiongozi wa chama mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe na Katibu Tawala Mkoa huo.

Alisema baada ya tukio hilo alikwenda kutoa taarifa katika kituo kikuu cha polisi Vwawa Machi 2, mwaka huu na kwamba polisi wanaendelea kuchunguza suala hilo.




Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Gullamhussein Kifu (katikati) akipokea msaada wa madawati, viti na meza 500 kwa ajili ya shule za wilaya hiyo, kutoka kwa Mkurugenzi wa Wateja wa Wadogo wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke, kwa ajili ya kuboresha sekta ya elimu wilayani. Wengine ni Mbunge wa Kibiti, Twaha Mpembenwe (kushoto), Mkurugenzi wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Neema Singo (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kibiti, Abduljabir Marombwa. **MPIGAPICHA WETU**

## Waziri ataka wahitimu kupewa vyeti kwa wakati

**Na Zuwena Shame**

SERIKALI imetoa wito kwa vyuo nchini kuharakisha utoaji wa vyeti kwa wahitimu wa fani mbalimbali ili kuwarahisishia utafutaji wa ajira baada ya kuhitimu masomo.

Aidha, serikali imesema kumekuwa na utaratibu kwa vyuo vingi nchini kuchelewesha utoaji wa vyeti kwa wahitimu na hivyo kuwafanya wengi wao kushindwa kuingia katika soko la ajira.

Wito huo ulitolewa jijini Dar es Salaam na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, wakati wa mahafali ya 19 ya Chuo cha Bandari.

Waziri alisema hayo baada ya Mkuu wa chuo hicho, Dk. Lufunyo Hussein, kusoma taarifa ya chuo, akisema kimedhamiria kutoa vyeti kwa wahitimu wake wa kozi za stashahada na astashahada ndani ya wiki moja.

Waziri Chamuriho alisema iwapo vyeti vitatolewa kwa muda mwafaka kwa wahitimu itarahisisha kuomba nafasi mbalimbali za ajira na kuongeza weledi katika shughuli zao kwani wengi wao wanakuwa na ari ya kufanya kazi.

"Wahitimu wengi wakimaliza vyuo wanahitaji vyeti ili kutafuta ajira, lakini wanakwama kutokana na vyeti hivyo kuchukua muda ... hii ni changamoto kubwa kwani wanashindwa kupata ajira kwa wakati mwafaka," alisema Waziri huyo.

# Rasimu muswada sheria ya bima ya afya yaiva




WIZARA wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imekamilisha rasimu ya Muswada wa kutunga sheria ya bima ya afya kwa wote ambao utawasilishwa Bungeni, Juni mwaka huu.

**Kwa sasa inaendelea kuandaa mpango utakaoruhusu maduka makubwa ya dawa kutoa huduma hiyo kwa wananchi wanaotumia bima ya afya.**

Aidha, imesema kwa sasa inaendelea kuandaa mpango utakaoruhusu maduka makubwa ya dawa kutoa huduma hiyo kwa wananchi wanaotumia bima ya afya.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Godwin Mollel, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Janeth Mahawanga.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji kwanini serikali isiruhusu maduka makubwa ya dawa kutoa huduma ya dawa kwa kutumia bima kwa wananchi.

Dk. Mollel alifafanua kuwa mpango huo upo na una utaratibu maalum kuwezesha maduka hayo kutoa huduma hiyo.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wajasiriamali wadogo kupata bima ya afya kupitia vikundi ambao ulikuwa msaada mkubwa sana kwenye Jamii.

Akijibu, Dk.Mollel alisema serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya inatoa kitita mahususi cha mafao kwa makundi maalum ya wajasiriamali ambao wamerasimisha shughuli zao kupitia mwamvuli wa jumuiya au vyama vyao vilivorasimishwa.

"Makundi ya wajasiriamali ambayo yananufaika na utaratibu wa bima ya afya ni pamoja na makundi ya wakulima kupitia vyama vya ushirika 225 vyenye idadi ya wanachama 6,196, vikundi 17 vya umoja wa wamachinga, wajasiriamali wadogo, wachimbaji wa madini," alisema.

Alitaja makundi mengine ni wavuvi, na mama lishe ambavyo vina idadi ya wanachama 2,315, na vikundi vya umoja wa madereva bodaboda na madereva wa malori na daladala ambavyo vina idadi ya wanachama 303.

Aidha, alisema kwa makundi ya wananchi ambao ni wajasiliamali lakini hawapo katika mwamvuli wa jumuiya za wajasiriamali zilizorasimishwa, mfuko umeanzisha vifurushi vya bima ya afya vya hiari ambavyo vinazingatia umri, ukubwa wa familia, aina ya huduma na gharama halisi za matibabu nchini.

Naibu Waziri huyo alifafanua kuwa hadi Machi, 31 2021 wanachama 32,343 wameshajiunga na mpango huu.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, akijadili jambo na mbunge wa Mwanakerekwe, Kassim Haji Kassim kwenye ukumbi wa bunge Jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Ataka barabara ya lami Kilyamatundu-Majimoto

MBUNGE wa Kwela (CCM), Deus Sangu, ameitaka serikali kuanza ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya kilometa 200 katika kutoka Kilyamatundu hadi Majimoto ambayo inaunganisha Mkoa wa Rukwa na Songwe.

Akiuliza maswali bungeni jana, Mbunge huyo alitoa angalizo kwa Wizara ya Ujenzi kuwa mtaalamu aliyepo eneo la mradi kasi yake ni ndogo sana na kutaka amalize kazi hiyo ndani ya kipindi cha mkataba.

"Kwa kuwa barabara kutoka Mji mdogo wa Laela kupitia Mlokola hadi kuunganisha nchi jirani ya Zambia ni ahadi aliyotoa Rais wakati wa kampeni, na wananchi wapo tayari kuachia eneo la barabara kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, naomba kujua lini barabara hii itafanyiwa upembuzi yakinifu ili ijengwe kwa kiwango cha lami,"alihoji.

Pia, alisema Hayati Dk.John Magufuli akiwa kwenye ziara Mkoa wa Rukwa aliahidi ujenzi wa barabara kutoka Kaengesa hadi Chitete na tayari upembuzi yakinifu umekamilika, na kuhoji lini ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami utaanza.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya alisema kuwa barabara ya Kilyamatundu – Muze – Mfinga – Kasansa hadi Majimoto yenye urefu wa kilometa 206 ni barabara ya mkoa inayosimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS).

Alisema kuwa barabara hii inaunganisha Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Songwe eneo la Kilyamatundu na Kamsamba katika daraja la Momba.

"Kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hiyo, Serikali ilianza kuchukua hatua za kuimarisha barabara hii kwa kuanza na kukamilisha ujenzi wa daraja la Momba lenye urefu wa mita 84 na barabara za maingilio zenye urefu wa kilometa 1.2 ambalo lilikuwa ni kikwazo kikubwa cha mawasiliano baina ya mikoa ya Rukwa, Katavi na Songwe,"alisema.

Aidha ,alisema serikali inaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu ambao unahusisha sehemu ya Kilyamatundu – Muze yenye urefu wa kilometa 142.

## Bil. 42/- zatengwa kuwalipa waliopisha umeme Chalinze

BUNGE limeelezwa kuwa Sh. bilioni 42.3 zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2021/22 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha mradi wa umeme Chalinze.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Chalinze(CCM), Ridhiwani Kikwete.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua ni lini wananchi hao watalipwa fidia kupisha ujenzi wa miundombinu ya miradi ya kusafirisha umeme kutoka Kinyerezi na Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Naibu Waziri Byabato akijibu swali hilo, alisema fidia ya wananchi hao itaanza kulipwa kuanzia Mwaka wa fedha 2021/22 baada ya taratibu zote kukamilika.

"Serikali kupitia TANESCO inatekeleza Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere hadi Chalinze na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme katika Kijiji cha Chaua - Chalinze,"alisema.

Alibainisha kuwa serikali kupitia TANESCO imekamilisha tathimini ya mali za wananchi na Taasisi zilizopisha utekelezaji wa mradi huu na fidia kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali.

Nipashe
# TESA
Jumanne Aprili 20, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 12



UHABA AJIRA ULIVYOIBUA VIJANA

ELIMU

# MAUAJI CHUKI ZA MAPENZI

- Kampeni ya kitaifa kulinda uhai yaweza kuwa mwarobaini

NA CHRISTINA MWAKANGALE

UKIUKWAJI wa haki ya kuishi, unaosababisha watu kuuliwa kikatili na wenza au wapenzi wao, unaelezwa na Ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2020, kuwa ni kitisho cha maisha kwa vile visa vya mauaji hayo vinaongezeka kila mwaka.

Ripoti hiyo inabainisha kuwa ukiukaji wa haki za binadamu unazidi kwenye haki ya kuishi, uhuru wa kujieleza na kutoa mawazo pamoja na haki ya kuwa huru.

Ni kwa mujibu wa Anna Henga, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) cha jijini Dar es Salaam, kinachoandaa ripoti hiyo.

Henga anasema hayo akiwasilisha muhtasari wa ripoti hiyo na kueleza kuwa kuna ongezeko la mauaji yatokanayo na wivu wa kimapenzi.

Anasema mauaji hayo yalifikia 23 mwaka jana, ikilinganishwa na 12 yaliyoripotiwa mwaka 2019.

Ripoti hiyo inabainisha kuwa matukio hayo yanakatisha haki ya kuishi, huku pia kukiwa na ongezeko la mauaji yatokanayo na kujichukulia sheria mkononi kutokana na wakati mwingine yakichochewa na imani za kishirikina.

Henga anasema mienendo ya hivi karibuni inaonyesha kwamba matukio ya wanawake kuuawa na wenza wao, yameongezeka kutokana na chuki na wivu wa kimapenzi, huku LHRC ikibaini kuwa mauaji hayo baadhi hufanywa na wenza wanaoishi pamoja au walioachana.

"Kwa mwaka 2019, LHRC ilikusanya matukio 12 ya mauaji ya wanawake yaliyofanywa na wenza wao, huku matukio nane yakihusishwa na wivu wa kimapenzi.

"Mwaka 2020, yalikuwa 32 yakihusisha mauaji ya wanawake yaliyofanywa na wenza wao, matukio 23 yalisababishwa na wivu na chuki za mapenzi. Mauaji haya ni ukatili dhidi ya wanawake na yanakiuka uhuru wao dhidi ya ukatili pamoja na haki ya kuishi," anasema Henga.



Mkurugenzi Mtendaji wa (LHRC), Anna Henga akizindua Ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2020, **PICHA: MTANDAO**.

> "Matukio hayo ni zaidi ya mara mbili ya yaliyotokea mwaka 2020, ikilinganishwa na yaliyoripotiwa mwaka 2019

"Matukio hayo ni zaidi ya mara mbili ya yaliyotokea mwaka 2020, ikilinganishwa yaliyoripotiwa mwaka 2019."

Pia, ripoti inaonyesha mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi yamepungua katika miaka ya hivi karibuni, taarifa za polisi zinaonyesha kwamba tangu mwaka 2015 wastani wa watu 640 wamekuwa wakiuawa na 'watu wenye hasira' kila mwaka.

SHERIA MKONONI

Henga anasena mwaka jana, polisi ilikusanya jumla ya matukio 443 ya mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi,

Mengi ya mauaji hayo yaliripotiwa katika mikoa ya Shinyanga, Katavi, Mwanza, Mbeya, Singida, Tabora, Simiyu,, Mbeya, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Pwani.

### UTAFITI

Henga anasema katika utafiti mdogo uliofanywa na LHRC kuhusu haki za binadamu, asilimia 27.2 ya washiriki walikubaliana na kauli kwamba mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi ni tatizo kubwa katika eneo wanaloishi au kufanyia kazi, huku asilimia 8.2 ya waliohojiwa ikisema wanakubaliana na kauli hiyo na asilimia 15.2 hawakukubaliani nayo.

Ripoti inaonyesha mauaji ya wanawake yanafanywa na wenza wao wa sasa na wa zamani, wakiwamo marafiki wao wa kiume wa sasa au zamani na wanaume zao.

Mwaka 2019, ripoti hiyo ya LHRC ilikusanya matukio 11 ya mauaji ya wanawake yaliyofanywa na wenza wao, huku matukio yakihusishwa na wivu wa kimapenzi.

Kwa mwaka 2020 mauaji hayo yalifikia 32 wanawake wakiuliwa na wenza wao, huku matukio 23 yakisababishwa na wivu wa kimapenzi.

Ripoti inabainisha kuwa mauaji hayo ni ukatili dhidi ya wanawake na yanakiuka uhuru wao pamoja na haki ya kuishi.

### NINI KIFANYIKE

Mapendekezo yaliyotolewa kwenye ripoti hiyo yana wasiwasi kwamba kuna hatari ya ukiukwaji wa haki za binadamu kwa watu kujichukulia sheria mkononi kuendelea.

Henga anawatahadharisha wananchi kujiepusha na vitendo hivyo na kuacha mfumo wa haki jinai uchukue mkondo wake.

"Kuna haja ya kuwaelimisha Watanzania kwa kuwa na kampeni ya kitaifa ya haki za binadamu ili kujua zaidi kuhusu athari za kujichukulia sheria mkononi, kuua wenza, wapenzi na kufahamu umuhimu wa uhai na maisha ili kuhakikisha tabia hiyo inakomeshwa."

Pia mapendekezo mengine ni kushughulikia changamoto ya rushwa katika mfumo wa haki jinai, ili kuimarisha imani ya wananchi kwenye mfumo huo.

ELIMU/UJASIRIAMALI

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Uhaba ajira ulivyoibua vijana kumiliki kiwanda

UHABA wa ajira rasmi nchini unaelezwa na vijana kuwa ni suala lenye pande mbili, wapo wanaoliita tatizo lakini kuna wengine wanaoliona kama ni fursa nyingine ya kiuwekezaji.

Ni uwanja mwingine wa kujitanua ki ujasiriamali, ndivyo wanavyoeleza baadhi ya vijana katika Manispaa ya Shinyanga, wanaotumia fursa hiyo kubadilisha maisha yao.

Wasomi 15 kutoka Shinyanga, wanaoiambia Nipashe kuwa baada ya kuishi bila ajira rasmi wamewekeza kwenye kiwanda kidogo cha kutengeneza chaki, watakazoziuza kwenye shule zilizoko mkoani Shinyanga.

Wanasema wanaamini katika kauli mbiu ya John Magufuli, ambaye enzi za uhai wake alipoingia madarakani 2015, alianza na sera ya Tanzania ya viwanda.

Ili kuibua wawekezaji hasa wanawake, vijana na wenye ulemavu, aliondoa riba kwenye mikopo inayotolewa na halmashauri akilenga kinamama, vijana, na wenye ulemavu.

Fedha hizo mitaji na kuanzisha biashara mbalimbali ikiwamo kufungua viwanda vidogo, kama walivyofanya wasomi hao.

Mwenyekiti wa kikundi hicho cha vijana 15 kinachojiita 'uzalendo na kazi, Hashimu Issa, anasema ukosefu wa ajira, ndiyo uliowasukuma kuanzisha mradi huo.

Anasema walibuni mradi wa kuanzisha kiwanda kidogo cha chaki kwa vile mkoa mzima wa Shinyanga hauna kiwanda hicho.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, (kushoto) akiangalia ubora wa chaki zinazotengenezwa na kikundi cha vijana 15 waliojiajiri kwa kuanzisha kiwanda cha chaki. **PICHA: MARCO MADUHU**

**WALIVYOIBUKA**

Issa anasema mara baada ya kuhitimu walitafakari na kuona kuwa ajira ni changamoto na kuanza kusaka mikakati ya kutoka ndipo wakapata wazo hilo la kiwanda cha kutengeneza chaki.

Baada ya wazo waliandaa katiba yao na kupeleka wazo hilo kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, ili kuomba mtaji kupitia fedha za mkopo kwa vijana , wanawake na wahitaji.

Issa anasema:

"Wazo lilikubalika na tulipata mkopo wa Sh. milioni 24.275 na hatimaye kuanzisha kiwanda hicho cha kutengeneza chaki mwaka jana, na sasa tunauza chaki kwenye shule zote za Manispaa ya Shinyanga, huku tukiendelea kutafuta masoko kwa shule zote za mkoa huu."

"Kama vijana ambao tumeamua kujiajiri wenyewe, tunaomba kuungwa mkono na serikali pamoja na walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari mkoani Shinyanga, kwa kununua chaki kutoka kiwandani kwetu ili tuinuke kiuchumi na kupanuka zaidi, na hatimaye kuongeza ajira nyingi zaidi kwa vijana,"anasema Issa.

"Mathalani, soko letu lipo hapa Manispaa ya Shinyanga pekee, tena baada ya kutolewa maagizo na mkurugenzi pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, kuwa shule zote wilayani hapa hakuna kununua chaki kwingine bali kwenye kiwanda chetu. Tunao uwezo wa kuhudumia shule zote za mkoa huu,"anaongeza.

> Nataka kila shule inunue boksi moja hadi mawili, chaki zipo za kutosha na vijana hawa wapo tayari kuwasambazia hadi kwenye shule zenu

Aidha, anatolea mfano mkoani Simiyu ambako Mkuu wa Mkoa, Athony Mtaka, aliagiza shule zote za mkoa kununua chaki kwenye kiwanda kilichopo wilayani Maswa mkoani humo, lengo likiwa ni kuwainua vijana waliowekeza kwenye mradi huo, kupunguza tatizo la ajira na kuchangia pato la taifa.

"Ndivyo hivyo tunavyotaka iwe kwa Shinyanga, wasiagize chaki nje kwani zipo zinazalishwa."

**FEDHA ZIPO**

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga Geoffrey Mwangulumbi, anasema:

"Vijana hawa walipokuja na wazo lao la kuanzisha kiwanda cha kutengeneza chaki, nikaona ni zuri sababu hapa mkoani kwetu hatuna kiwanda hicho, hivyo sikusita kuwapatia fedha za mkopo wa milioni 24.2 kwa ajili ya mtaji na kuanza uzalishaji wa chaki."

Anaeleza kuwa halmashauri hiyo ina fedha nyingi za mikopo bila riba na kuwataka vijana wajiunge kwenye vikundi na kupeleka mawazo yao ya biashara ambazo zinauzika sokoni, ili wasikwame bali wainuke kiuchumi na kuendesha maisha yao.

"Msaada wangu kwao vijana hawa nikiwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, nilitoa maagizo kwa mdomo na maandishi kwa walimu wote wa shule za msingi na sekondari wasinunue chaki kwingine bali kwenye kiwanda hiki cha vijana ili tuwaunge mkono na ndiko wanaponunua chaki,"anaongeza Mwangulumbi.

**WILAYA KUSAKA SOKO**

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anasema mara baada ya kutembelea kiwanda hicho cha kutengeneza chaki, alifurahishwa na namna vijana hao walivyoibua wazo zuri, naye pia alitoa maagizo kwa shule zote za Wilaya ya Shinyanga, zinunue chaki kutoka kwenye kiwanda hicho ili kuwainua vijana hao kiuchumi.

Anasema vijana wanapoanzisha jambo lenye tija na kujiajiri wenyewe ni vyema wakaungwa mkono, na ndivyo hivyo anavyofanya na licha ya kutoa maagizo kwa walimu wakuu wote wa shule za msingi na sekondari wilayani humo kununua chaki kiwandani hapo, pia ataendelea kuwatafutia soko kwenye halmashauri nyingine za Shinyanga.

"Nawaagiza wakuu wa shule zote watumie chaki zinazozalishwa katika kiwanda chetu cha Shinyanga, kuna chaki za kutosha nataka zinunuliwe. Hatuwezi kununua nje ya Shinyanga wakati tunazo hapa kwetu kwenye kiwanda chetu, tena ni nzuri sana na vijana wanafuata taratibu zote za uzalishaji", anasema Mboneko.

"Nataka kila shule inunue boksi moja hadi mawili, chaki zipo za kutosha na vijana hawa wapo tayari kuwasambazia hadi kwenye shule zenu,"anaongeza Mboneko.

Mbunge wa Viti Maalumu mkoani Shinyanga, Santieli Kirumba, ambaye alitembelea kiwanda hicho anawapongeza vijana hao na kuwapatia Sh. 250,000 kama mchango wake wa kuwaunga mkono katika kuendeleza Tanzania ya viwanda.

"Nawapongeza vijana kwa uthubutu wao wa kuanzisha kiwanda hiki cha kutengeneza chaki, na wasikate tamaa licha ya kukabiliwa na changamoto ya kukosa soko la uhakika, bali waendelee kutengeneza bidhaa bora na zenye kiwango," anasema Kirumba.

Ofisa Vijana Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga Charles Luchagula, akizungumza kwa niaba ya Ofisa Maendeleo ya Jamii John Tesha, anasema tangu mwaka 2015 hadi 2020, manispaa hiyo imetoa mikopo kwa vijana inayofikia Sh. milioni 524 kwa vikundi 48.

Anasema kwa mwaka huu wanatarajia kutoa tena fedha hizo za mikopo kwa kinamama, vijana na wenye ulemavu akiwataka wadau wa makundi hayo wachangamkie fursa hiyo ya fedha za halmashauri, kwa kujiunga kwenye vikundi ili wapate mitaji na kufanya uwekezaji ili kujiingizia kipato.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Hilo ndilo jambo la wanaoishi na ulemavu kwa Rais Samia

BAADA ya Rais, Samia Suluhu Hassan, kuchukua usukani wa kuliongoza taifa, Watanzania wanaendelea kuona kuwa anagusa mioyo ya wengi na ataendelea kutetea wote hasa walioachwa pembezo ili wasonge mbele kufikia maendeleo ya taifa.

Katika makala hii, Nipashe inazungumza na Eligius Bwalya, ambaye ana ulemavu wa aina mbili unaohusisha viungo na macho, kujua kile kundi hilo linachotamani kimfikie Rais.

Bwalya ni mwalimu mwenye shahada ya uzamili ya watu wenye mahitaji maalumu (Master of Education in Special Education), na sasa ni mtumishi wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) jijini Dar es Salaam, kwenye eneo la uandishi wa mitaala.

Mwalimu Bwalya anaeleza, kile ambacho anahisi ni matamanio yake na ya wenye ulemavu kwa Rais Samia na hata kile anachodhani wangetaka Ikulu iwafanyie.

Katika mahojiano hayo, Bwalya anatamani kuona wenye mahitaji maalumu wakiteuliwa katika kila uteuzi Rais Samia anaofanya. Anaanza...



Balozi wa Tanzania nchini Vatican, Dk Abdallah Possi ni miongoni mwa wawakilishi walioteuliwa na Ikulu kuwakilisha nchi ughaibuni. **PICHA: MTANDAO**

> Ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuna kundi la watu wenye ulemavu. Hili kundi tungeweza kuliweka kwenye Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, lakini kwa unyeti wake tumelinyanyua tukaliweka Ofisi ya Waziri Mkuu.

**SWALI: Ni kitu gani ungependa kuona Rais akifanya kwa ajili ya wenye uhitaji maalumu?**

**JIBU:** Ningependa kuona kuna Mkuu wa Wilaya, Mkoa, Kamishna wa Tume ya Uchaguzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala au Mamlaka za Udhibiti mwenye ulemavu akipewa jukumu hilo.

**SWALI:Ni kitu gani kinachokusukuma kuwa na matamanio hayo?**

**JIBU:** Niinukuu hotuba yake ambayo wenye ulemavu wanasimamia . Hii ni sehemu ya hotuba ya Rais, akizungumza Aprili 06, 2021 wakati wa kuwaapisha baadhi ya wateule wake, anataja haya:

“Ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuna kundi la watu wenye ulemavu. Hili kundi tungeweza kuliweka kwenye Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, lakini kwa unyeti wake tumelinyanyua tukaliweka Ofisi ya Waziri Mkuu.

“Naomba mkawashughulikie, hawa watu wana manung'uniko mengi sana. Wasikilizwe na yanayowezekana yatekelezwe, yasiyowezekana yaletwe huku juu tuzungumze kwa pamoja...”,

Nami Bwalya naanza kuchangia katika yale watakayozungumza, hili la uteuzi ni sehemu ya mambo yanayotakiwa yafikishwe mezani kwake kwa mazungumzo.

Hotuba hiyo inaleta matumaini kuwa Rais anawakumbuka watu wanaoishi na ulemavu.

“Hata sisi watu wenye ulemavu tuko kwenye mipango yake. Jambo ninaloweza kumwomba Rais ni kwamba wenye ulemavu wangependa kuwa na uwiano na uwakilishi mkubwa katika kila sekta.

“Hii ni kutoka na ukweli kuwa serikalini kuna nafasi nyingi sana ambazo tungefurahi kuona tunachomoza kila mahali.”Mara nyingi huwa napenda kusema kuwa sayansi ya jamii imewaweka walemavu, wanawake, wazee, wakimbizi, yatima na watoto kwenye kundi moja ambalo wanaitwa ‘the disadvantaged group’.

Lakini, ukiangalia makundi yote haya, kundi la wanawake limepiga hatua kubwa.

“Kwa sasa siyo wenzetu tena. Kila nafasi zilizoko serikalini, wanawake wamechomoza kuanzia urais, uwaziri, ukuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, waganga wakuu wa mikoa na wilaya, wakurugenzi wa bodi, wakuu wa vyuo, vyuo vikuu na taasisi mbalimbali za serikali”

“Ni makatibu tawala wa mikoa na wilaya, majaji, viongozi jeshini kama makamanda wa mikoa na wakuu mfano Uhamiaji, mabalozi nje na ndani ya nchi, wabunge na nafasi nyingine za kiutendaji na kiutawala. Kote huko wanawake wameng'ara na hakuna mahali, iwe bungeni, serikalini, ubalozini, mahakamani ambako hutakuta mwanamama.

**SWALI: Unadhani ni kwanini kumekuwa na mafanikio hayo?**

**JIBU:** Hii haijaja kwa bahati mbaya bali ni matokeo ya juhudi za makusudi za dunia kuwainua wanawake .

Tukirejea Mkutano wa Beijing China wa mwaka 1995 ndiyo ulioanzisha ajenda hiyo pia Tanzania kuwapo kwa taasisi za kuhamasisha na kupiga kelele kwenye vyombo vya habari kama Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA) na Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA) na vyote vinahamasisha kuhusu haki za wanawake kushiriki na kuwa sehemu ya uamuzi.

Tungependa hata hili litokee kwetu wenye ulemavu.

**SWALI: Idadi ya wanawake duniani na hata Tanzania ni kubwa kuliko ya wanaume, kwa hiyo kuwaacha nyuma ni jambo lililopingwa si hapa nchini hata kwingineko duniani, pengine huoni kuwa haiwezekani idadi ya wenye ulemavu haiweza kulinganishwa na wanawake, tuambie idadi ya wenye ulemavu hapa Tanzania wanaweza kuwa wangapi?**

**JIBU:** Kwa mujibu wa Shirika la Afya la Duniani (WHO), kila penye Watanzania 10, mmoja ni mlemavu. Hivyo basi, tunaweza kuwa na walemavu takribani 6,000,000 ambao tungependa kuwakilishwa katika kila nafasi kwenye nyadhaifa za uongozi wa serikalini.

Kwa hiyo tunamuomba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atukumbuke katika kila nafasi aliyo na mamlaka ya uteuzi.

“Tunatamani kuwaona walemavu wakichomoza katika ngazi za mawaziri na manaibu waziri, makatibu wakuu na manaibu, wakuu wa taasisi mbalimbali za serikali, wakuu wa mikoa na wilaya, makatibu tawala wa mikoa na wilaya, majaji, wabunge, wakurugenzi wa halmashauri, mabalozi, makatibu wakuu, wakuu wa vyuo na vyuo vikuu na ngazi nyinginezo.”

Pia uteuzi wa wanaoishi na ulemavu katika sekta mbalimbali usiishie kwa Rais pekee ,bali awahimize wasaidizi wake wenye mamlaka na uteuzi kama mawaziri na makatibu waku wao wahakikishe wanawateua walemavu katika kila nafasi zilizo na mamlakanazo.

Kwa kufanya hivyo, jamii itawatambua watu wenye ulemavu na hivyo kuondoa mawazo potofu kuwa ukishakuwa mlemavu, maana yake umeshindwa maisha na huwezi kitu.

Pia itawaamsha wazazi wanaowaficha watoto wenye ulemavu na kuwapeleka shuleni.

Naomba nimalizie kwa kusema kuwa hatujachelewa sana, muda tunao na wakati ni sasa.

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Kukuza Kiswahili kunapotatizwa na zama mpya, uchumi shindani

WAKATI ulipotangazwa mkakati wa kukuza Kiswahili katika nyanja tofauti za kiutawala na kijamii, ambao kimsingi bado upo, uzoefu ulionyesha kuwa suala hilo halitafuatiliwa bila ushindani, kwani Kiswahili hakimsaidii kijana kupata ajira, ila Kiingereza ni muhimu zaidi.

Ujuzi wa Kiswahili ni nyenzo shindani katika ajira kwa maeneo machache hasa yanayohusiana na habari au ushereheshaji au upambaniaji kwa watu wa kawaida vifaa au nyenzo za kiufundi katika eneo fulani, kwa mfano dawa za aina tofauti iwe ni za kilimo (zinaitwa viuatilifu).

Hasa ni lugha ya kuzungumzia kinachohusika, si kukielewa.Kujua kwa undani bidhaa au nyenzo husika iko vipi , imetengenezwaje, ina matumizi ya aina zipi na kwa uangalifu kiasi gani lazima kurudi katika lugha ya awali ya kiteknolojia, kujua viini vya kemia au anuwai' vilivyotumika.

Suala hapa ni kwamba kinachohitajiwa siyo tu kufahamu viini au chembe husika kwa majina yake ila pia mengine kitaaluma, kwani kujua vianzio hivyo, maingiliano yake ndiyo inawezesha kuelewa tahadhari au taratibu, mipaka ya matumizi husika, kufafanua tatizo linapotokea.

Kutojua viini kunaleta kukariri, yaani mtu aongee kwa Kiswahili nini alicholeta pale ila hana uelewa wa kina wa mifumo iliyotumika kukiunda, au miiko yake katika matumizi na sababu zake.

Maeneo hayo ya matumizi ya lugha katika kujifunza fani tofauti shuleni na vyuoni, tofauti na kutumia uelewa huo kueneza masuala kadhaa ya kiufundi miongoni mwa watumiaji yalikuwapo hata katika kufikiria ukuzaji wa Kiswahili wakati huu uliopita.

Sasa kuna mabadiliko kutokana na kuiacha dira ya uchumi unaojiangalia ndani kwa ndani na kuhitaji wawekezaji kwa maneno huku mkazo ukiwe kwenye hisia potofu kuwa wawekezaji wageni wanafaidi zaidi kuliko nchi.

Kuna mabadiliko katika mwelekeo wa usimamizi sera, kwa kutambua tunawahitaji wawekezaji kuliko wao wanavyotuhitaji, kwani unaweza kuhamishia mitaji kokote ambako kuna amani, si rasilimali, nguvu kazi.


Hivi sasa kuna mkasa wa kuingia kwa mahindi ya Tanzania nchini Kenya ila kwa magendo, na sababu mojawapo inayoonekana ni kuwa uzalishaji hapa nchini umechukulia soko la mahindi Kenya kama kitu kinachotazamiwa au kinafahamika kipo, siyo cha kuulizia. Tatizo ni kuwa Tanzania imekataa kuingia mkataba halisi wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki ambalo ni mojawapo ya hatua za kujenga umoja wa kiuchumi wa eneo hili, ikiridhia kikamilifu Umoja wa Forodha, kitu kikiagizwa kutoka nje na kuingia nchi mojawapo, kisitozwe kodi nyingine. Pia nchi hizi zinaoanisha viwango vya ushuru kabla ya bajeti.

Ukisikiliza kinachosemwa katika suala la kilimo cha biashara na hata viwanda vyenye msingi wake katika bidhaa za kilimo, unakuta kuna matazamio yasiyo haba ya kutumia masoko ya nchi jirani kama sehemu mahsusi ya dhana ya soko ambayo yanakuwapo katika uzalishaji.

Ina maana kuwa endapo Tanzania inakuwa wawekezaji waje nchini, licha tu ya kuongeza uzalishaji katika maeneo tofauti ndani ya nchi, ina maanisha vijana wanaomaliza sekondari na vyuo watahitajika kuwa na uwezo wa kujitambulisha kwa wageni na kuongea hata kama ni kwa uchache kiasi fulani.

Kutokana na udhaifu mkubwa wa kuongea lugha ya Kiingereza hapa nchini, hilo linahitaji kuwekewa mkazo maalum.

Ina maana pia kuwa ili vijana wapate ajira za hapa na pale katika viwanda vidogo maeneo ya wilaya au mikoa, mafunzo ya kiufundi inabidi yapewe kipaumbele, iwe ni katika kilimo, ufumaji, umeme, injini za aina tofauti na hasa inapogusa kompyuta (labda kuna Kiswahili chake).



Utaalamu na teknolojia unahusisha utambuzi na ugunduzi wa vitu kuanzia taarifa na maelezo muhimu, majina na muingiliano na kazi nyingi zimetumia Kiingereza. Kiswahili hakiwezi kuzipa majina sehemu zote za mwili wa binadamu kazi ambayo ilifanywa miaka mingi iliyopita. Itakuwaje ikielekezwa kutumia lugha hiyo kufundisha elimu ya viumbe hai kuanzia msingi hadi vyuoni? **PICHA: MTANDAO.**

Ina maana kuwa vijana watahitaji kupata uzoefu wa vielelezo vya kiufundi na hata vya kitaaluma katika umri mdogo, kidogo zaidi shule za msingi lakini zaidi sekondari.

Inamaanisha kuwa kusoma kwa Kiingereza kuwekewe mkazo zaidi ili kuwe na usawa kiasi fulani katika kufatuta ajira halisi au za kujikimu, kile kinachoitwa kujiajiri, dhana ambayo ni kosa kisanifu, au labda ni 'kumsanifu' mbangaizaji kuwa 'anajiajiri,' wakati kimsingi anatafuta ajira.

Endapo matazamio yaliyoainishwa na serikali ya kimapinduzi iliyotangulia kuona Kiingereza kama vile ni 'mabaki ya ukoloni' yatafuatiliwa ("kabla hata Mzungu hajafika unasikia mtu,'you know.....," halafu watu wanacheka) ina maana ajira zote zenye ladha zitaenda kwa wanaosoma 'English Medium' na karo zake zitapanda kwa kiwango kikubwa kwani wazazi watapigania watoto wao wasome huko.

Ni ili wawe na msingi unaokubalika wa kutafuta ajira za kujikimu baada ya masomo ya sekondari. Uwepo wa wageni wengi katika kuuza bidhaa, kusafiri nchi za jirani na kupokea bidhaa za kila aina na kuhitaji kuzitumia, kwa mfano vifaa vya simu, kompyuta na mengine ni mazingira ya kila siku yanayohitaji kujua Kiingereza ili kushiriki shughuli yoyote hata iwe ni kando tu ya barabara. Watu 'hawatadanganyika' na Kiswahili.

Wakati akiwa makamu wa rais kiongozi mkuu wa sasa alisema tuhamie Kiswahili ili watu wasikose haki zao kwa kutojua lugha, ikaelezwa kuwa mahakama za mwanzo hutumia Kiswahili kwa shughuli zote na sehemu kubwa ya kuendesha mashauri mahakama za wilaya. Inapokuja katika mahakama za kibiashara, Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani, kuna mivutano ya kisheria ambako ni wanasheria wanavutana na siyo mwananchi wa kawaida anayefuatilia haki yake.

Maelezo hayo yaliendana na vipaumbele vya sera na 'mageuzi ya kitamaduni' ya kutusahaulisha mambo ya Magharibi ikiwa ni pamoja na mikutano mingi mno kati ya makundi ya hapa nchini na yale ya nchi za Ulaya au katika ukanda huu.

Ni mwelekeo ambao sasa hauna mashiko kwani uchumi shindani unachanganya washiriki toka popote, hivyo kuhitaji kuinua vipaji na kujenga ufasaha wa lugha ya kuelezea vipaji hivyo na lugha shindanishi ni Kiingereza.



## Bashungwa ataka ubunifu watumishi Wizara ya Habari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, ametaka watumishi wa wizara hiyo kuwa wabunifu katika kutekeleza majukumu yao hatua inayoboresha utendaji kazi na kufikia malengo ya serikali.

Bashungwa aliyasema hayo jijini hapa katika kikao cha wafanyakazi wa wizara hiyo chenye lengo la kuwakaribisha viongozi wapya pamoja na kufanya kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo.

Alisisitiza upendo, uaminifu, ushirikiano, kuchapa kazi kwa weledi na kuongeza ubunifu katika kazi wanazofanya kwa maslahi ya taifa.

Alisisitiza kuwa viongozi na watumishi wa wizara hiyo ni lazima kufanya kazi kwa bidii na jitihada katika maeneo yao ya kazi kwa kuungaanisha nguvu kwa kuwa wanasifa kwenye nafasi zao ili wizara hiyo ifike mbali zaidi katika kuwatumikia Watanzania.

"Naamini katika ushirikiano, sisi viongozi wenu tunachotarajia ni kuona mnaendelea kuwa wazalendo, wachapakazi, wabunifu na kuwa watu mnaowekeza katika bidii ya utendaji na sio majungu, fitina na uzembe kazini," alisema.

Hata hivyo, Waziri Bashungwa alisema wizara yake tayari imetekeleza maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu kufungulia vyombo vya habari husasan Tv mtandao na maagizo hayo wameyatekeleza kwa kushirikiana na Wizara ya Habari na Teknolojia ya Mawasiliano kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Kwa upande wake, Naibu Waziri katika wizara hiyo, Pauline Gekul, alimshukuru Rais Samia kwa kumwamini na kumteua katika nafasi hiyo na kuahidi kumpa ushirikiano na kutoa matokeo anayotarajia.

Alisisitiza watumishi hao kushirikiana katika kufanya kazi kwasababu wizara hiyo ni nyeti na inagusa maisha ya watu kupitia sekta zake na kuikumbusha jamii kuzingatia utamaduni pamoja na kuimarisha na kuenzi mila na desturi za nchi.

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Hassan Abbasi, alisema bajeti ya wizara inaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Alisema kwa mwaka ujao wa fedha wa 2021/2022, inatarajia kuwa na ongezeko la bajeti ya fedha za maendeleo kufikia Sh. bilioni 20 kutoka Sh. bilioni 7.7 mwaka uliopita.

Pia, alisema fedha za matumizi mengine zimeongezeka kutoka Sh. bilioni 11 kwa mwaka 2020/2021 na inatarajiwa kufikia Sh. bilioni 14 kwa mwaka ujao wa fedha 2021/2022 ambazo zimetengwa kutekeleza majukumu ya Wizara hiyo.

# Wakazi Dodoma watakiwa kuchangamkia elimu BRELA

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Bilinith Mahenge, amewataka wakazi wa mkoa huo kuchangamkia elimu inayotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kwa kuwa ina umuhimu mkubwa katika kujikwamua kiuchumi.

Dk. Mahenge aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa wakazi wa jiji hilo.

Akizungumza katika ufunguzi huo, Dk. Mahenge aliwaambia washiriki kwamba ili kufanikiwa ni vyema biashara au kazi husika ikarasimishwa na kutambulika kisheria.

"Hatua ya kwanza ya kufanikiwa katika biashara ni kuirasimisha biashara ili itambulike kwa mujibu wa sheria. BRELA wapo hapa Dodoma kwa siku mbili kwa hiyo hii ni fursa kubwa na adhimu," alisema Dk. Mahenge.

Naye, Msimamizi wa Kanda ya kati na Ofisi ya BRELA mkoani Dodoma, Gabriel Girangay alisema licha ya elimu hii kwa wote inayotolewa kwa siku mbili, lakini pia ofisi zipo tayari kwa ajili ya kuwahudumia.

"Ofisi ya BRELA mkoani Dodoma ipo tayari kuwahudumia na inafanya maandalizi ya kufika katika wilaya zote tisa za Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi katika maeneo yao kuhusu huduma zetu," alisema Girangay.

Aliwataka pia wadau wa BRELA walio katika mkoa huo na kanda nzima ya kati, wasipate shida ya kwenda ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam na badala yake wafike katika ofisi za BRELA mkoani hapo katika jengo la PSSSF Makole, ghorofa ya 10.

Naye Msaidizi wa Ofisi Mwandamizi wa Utawala kutoka BRELA, Saada Kilabula, alimshukuru Mkuu wa mkoa kwa niaba ya Ofisa Mtendaji Mkuu, Godfrey Nyaisa kwa kuthamini uwapo wao ndani ya Dodoma na kuja kufungua mafunzo hayo.

BRELA inaendelea na mpango wa kutoa elimu kwa umma, awamu ya kwanza mikoa sita itafikiwa ambayo ni Ruvuma, Njombe, Iringa, Singida, Dodoma na Morogoro.



Katibu wa Kanda ya Kati Dodoma, Chifu wa Mazengo Kamwaya, Ashery Maloda, akiwaonyesha idadi ya machifu wanaotambuliwa miongoni mwa makabila yenye machifu, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) jana, Dodoma, kuhusu kuibuka kwa watu wanaojipachika cheo cha uchifu wakati hawana vigezo wala sifa zinazotakiwa kushika nafasi hiyo yenye heshima kubwa. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Serikali yatambua juhudi elimu kwa watoto wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imesema inatambua juhudi kubwa zinazofanywa katika mradi wa elimu maalum kwa watoto wenye ulemavu wa akili uliolenga kuwapatia mahitaji yao stahiki ili wafikie malengo yao.

Ofisa Elimu Maalumu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Seleman Chamshama, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na maofisa elimu maalumu na walimu wa vitengo vya watoto wenye ulemavu wa akili jijini hapa.

"Tunatambua kuwa watoto hao wenye ulemavu wa akili wana changamoto nyingi, lakini hata hivyo serikali haipo nyuma kuhakikisha matatizo yao yanatatuliwa, hii ni pamoja na mashirika, taasisi na watu binafsi ambao wanaojitolea kwa ajili ya watoto hao, hivyo nasema tutahakikisha wanapata mahitaji yao hayo kama ilivyo kwa wenzao ambao hawana ulemavu," alisema.

Awali, akizungumza kwenye mafunzo hayo Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Special Olympic inayojihusisha na Elimu Jumuishi kwa ajili ya watoto wenye ulemavu wa akili, Charles Rays, alisema bado kuna tatizo watoto hao kukosa mahitaji yao stahiki kama ilivyo kwa wenzao.Mkurugenzi huyo ambaye Shirika lake limefadhiliwa na Stavros Niarchos Foundation, alisema watoto hao wenye ulemavu wamekosa mahitaji muhimu kama vile miundombinu ya viwanja vya michezo, vifaa visaidizi, matibabu elimu na hata kushirikishwa kwenye jamii.Naye, Mwalimu wa kitengo cha elimu maalum kwa ajili ya watoto wenye ulemavu wa akili Shule ya Msingi Mlezi Jiji la Dodoma, Edinesta Tati, aliiomba serikali kuwaangalia watoto hao kutokana na mazingira waliyonayo kwenye maisha yao ya kila siku.

Alitaja mazingira hayo ni pamoja na ukosefu wa viwanja vya michezo ili waweze kushiriki kwenye mashindano mbalimbali yakiwamo ya kimataifa na kitaifa.





## Wanafunzi sasa wapata vyoo vya kisasa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAFUNZI wa shule za msingi Lusungo na Nsambya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, ambao walikuwa wanajisaidia vichakani kwa sababu ya kutokuwa na vyoo, wameondokana na kero hiyo, baada ya kujengewa vyoo vya kisasa.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kupitia mradi wa SAWA, iliamua kufadhili mradi wa ujenzi wa vyoo bora katika shule hizo.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Lusungo, Kanuti Mbamba, alisema awali walikuwa na jumla ya matundu sita ya vyoo ambao matatu yakiwa wavulana na matatu vya wasichana.

Alisema kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi ukilinganisha na matundu ya vyoo vilivyopo wakati wa mapumziko wanalazimika kwenda vichakani kujisaidia.

Alisema Shirika la UNICEF kupitia mradi wa SAWA wamesaidiwa kujengewa matundu zaidi ya 26 ya vyoo.

"Hali ilikuwa mbaya kwa watoto wetu kutokana na uhaba wa vyoo walilazimika kujisadia vichakani tulikuwa na matundu matatu ya wavulana na wasichana ambayo kipindi yalikuwa hatoshi na kusababisha foleni kubwa, baada ya UNICEF kupata taarifa juu ya adha hii waliamua kutufadhili kujenga matundu 20 kwa shule yetu," alisema Mbamba.

Mwanafunzi wa Shule ya Nsambya, Claud Bahati, alisema walikuwa wanatumia magunzi na majani kujisaidia kutokana na vyoo hivyo kutokuwa na miundombinu ya maji lakini hata walipoenda vichakani.

Alisema baada ya kujengewa vyoo bora na UNICEF wanajisaidia chooni, huku wakitumia maji safi na salama.

Mkurugenzi wa Mradi wa SAWA, Charles Zakaria, alisema Shirika la UNICEF limejikita kuboresha miundombinu ya elimu kwa watoto kwa kuhakikisha kuna kuwa na usafi wa mazingira na huduma za maji ili kuboresha afya za watoto.

Alisema ujenzi huo umegharimu zaidi ya Sh. milioni 76 ikijumlisha gharama za saruji, mbao, gharama za mafundi, huku wananchi kupitia nguvu kazi zao wakichangia Sh. milioni mbili.

# Serikali yakerwa migogoro Chunya

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya, imekerwa na baadhi ya wananchi wilayani humo kuzusha migogoro inayohatarisha amani kwenye jamii ikiwemo inayohusu wawekezaji.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Saimon Mayeka, alionyesha kukerwa na tabia hiyo juzi alipokuwa anasuluhisha mgogoro kati ya wananchi na mwekezaji anayechimba dhahabu kwenye eneo la Mlima Kaputa ambapo wananchi wanataka mwekezaji huyo aondolewe.

Alisema wananchi wa kijiji hicho walitengeneza maneneo ya uongo wakati wa Ziara ya aliyekuwa Rais wa wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli wilayani humo Mei 2019 wakidai mwekezaji wa eneo hilo anakiuka sheria.

Alisema wananchi hao walimwambia Hayati Dk. Magufuli kwamba mwekezaji huyo anachimba madini kwenye eneo lenye matengi ya maji pamoja na eneo lililotengwa kwa ajili ya makaburi, jambo ambalo alisema ilikuwa ni uongo.

"Suala la kumdanganya rais siyo jambo dogo ndugu zangu, sasa mkishindwa kulimaliza jambo hili tutatoa uamuzi wa mwisho wa serikali, maana serikali ni zaidi ya kijiji chenu," alisema Mayeka.

Ofisa Madini Mkazi wa Wilaya ya Chunya, Sabai Nyansiri, alisema wananchi hao wamekuwa wakimtuhumu mwekezaji wa eneo hilo ajulikanaye kwa jina la Jose Mwazyele kuwa anamiliki mlima mzima wa Kaputa jambo ambalo sio kweli.

Alisema Serikali haina mpango wa kummilikisha mwekezaji huyo mlima mzima na badala yake wananchi wote wanaohitaji kuwekeza kwenye sekta ya madini watapewa nafasi kwenye eneo hilo.

"Eneo la Mwazyele ni dogo sana lakini lengo la serikali ni kuwanufaisha wananchi wote wa Tanzania na hata ninyi mtanufaika endapo mtakuwa tayari kuwekeza kwenye eneo hili," alisema Nyansiri.

Hata hivyo, baadhi ya wakazi wa eneo hilo walikiri kuwa maelezo waliyopatia Dk. Magufuli yalikuwa ya uongo na yalisababisha mwekezaji wa eneo hilo kushindwa kuendelea na kazi yake ya kuchimba madini.

Mangazin Zambi alisema maelezo yote ambayo yalitolewa kuwa mwekezaji huyo anachimba kwenye vyanzo vya maji na makaburini yalikuwa siyo ya kweli.

Naye Mussa Kagoba, alisema wao hawakuwa na nia ya kumdanganya rais, na kwamba kilichofanyika ni maelezo yao kunukuliwa tofauti huku akidai kuwa wao walitaka kueleza kuwa mwekezaji huyo alikuwa anawanyanyasa wananchi.

Alisema kinachowasumbua wananchi wa kata hiyo ni makundi ya siasa kuwagawa na kwamba hayo ndiyo yamekuwa yakipandikiza chuki miongoni mwa wananchi.

Diwani wa Kata ya Chalangwa, Haji Chapa, alisema kutokana na mgogoro huo imefika mahali wananchi wa Kata hiyo wamekuwa wakiwatishia maisha viongozi wa Serikali akiwemo na yeye mwenyewe.

Alisema baadhi ya wananchi hao walikuwa wanamtuhumu kuwa alipewa Sh. milioni 30 na Mwazyele ili amtetee na kwamba walifikia hatua wakabonda gari lake na kupasua vioo wakati ameegesha sehemu.

"Mimi sijashiriki kwenye jambo hilo, lakini imefika mahali mmepiga mawe gari langu na sielewi ni nani, nawaombeni wananchi tuache hizi tabia hazitatufikisha popote," alisema Chapa.

Wilaya ya Chunya ni miongoni mwa wilaya zinazokabiliwa na migogoro mingi baina ya wachimbaji wadogo na wawekezaji hali ambayo wakati mwingine huwa inasababisha uvunjifu wa amani.



Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Dk. Yahya Msuya, akitoa maelezo ya namna ya unawaji kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Nsambya iliyopo katika Kata ya Iwindi wilayani humo, wakati Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa mataifa (UNICEF) lilipokuwa linakabidhi matundu ya vyoo kwa ajili ya shule hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Zana duni zaharibu ubora wa maharagwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa wakulima wa maharage katika mikoa ya Mbeya na Songwe wanapunguza ubora wa mazao yao wakati wa kuvuna kwa kuyapasua wanapopiga na kushindwa kuyakausha kwa ubora kutokana na kutumia zana duni.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Dk. Tulole Bucheyeki, wakati taasisi hiyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha mazao ya kitropiki la CIAT zilipokabidhi mashine za kisasa kwa vikundi viwili vya wakulima wa zao hilo.

Vikundi vilivyokabidhiwa mashine hizo ni kikundi cha wanawake cha Mshewe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kikundi cha Upendo kilichopo Kata ya Senjele wilayani Mbozi katika Mkoa wa Songwe.

Mashine zilizokabidhiwa kwa vikundi hivyo ni mashine maalumu ya kupigapiga maharagwe na mtambo maalumu wa kukaushia maharagwe unaotumia nishati ya Jua (Bean Solar Drier).

Alisema wakati wa kuvuna wakulima wengi wanapigapiga maharage yao kwa kutumia njia za kienyeji hasa kutumia fimbo hali ambayo husababisha mazao yao kupasukapasuka na hivyo kupungua thamani.

"Lakini pia wakulima wengi mazao yao huwa yanaoza kutokana na kutokaushwa vizuri na hivyo kuyafanya yasiuzike ama bei yake kuwa chini kuliko vile ambavyo wao huwa wanatarajia na haya ni matatizo ambayo yanawakabili wakulima wengi katika mikoa yetu," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema katika utafiti waliofanya hivi karibuni walibaini kuwa wakulima wanapoteza kati ya asilimia 25 na 80 ya mazao yao wakati wa michakato hiyo miwili ambayo ni mchakato wa kupigapiga na kukausha.

Mwakilishi wa Shirika la CIAT, Sylvia Karemera, alisema walikabidhi mashine hizo kwa vikundi vya wakulima hao ili kuwapunguzia mzigo wakati wa shughuli hizo pamoja na kuongeza thamani ya mazao yao kwa kuepusha mazao kuoza na kupasuka. Alisema kwenye shughuli za kupiga na kukausha mazao hayo wanaoumia zaidi ni wanawake na watoto na kwamba ndio maana walishawishika kusaidia vikundi hivyo.

"Wakati mwingine wakulima wanavuna maharage yao wakati ambao hali ya hewa sio nzuri na hivyo kushindwa kuyakausha vizuri, sasa sisi kama wadau tumeamua kuwasaidia mashine hizi ili ziwapunguzie kazi," alisema Sylvia.

Alisema mashine ya kupigapiga maharage ina uwezo wa kupiga aina nane za mazao yakiwamo mahindi na hivyo akawataka wakulima hao kuzitumia vizuri mashine hizo.

Baadhi ya wakulima waliokabidhiwa mashine hizo walizishukuru taasisi hizo kwa kuwasaidiwa wakidai kuwa mashine hizo zitawasaidia kupunguza kasi pamoja na kuongeza thamani ya mazao yao.

Mwenyekiti wa Kikundi cha wakulima cha Upendo wilayani Mbozi, Daud Bukuku, alisema baada ya kupatiwa mashine hizo watavuna mazao yao kwa wakati na kuyauza kwa bei yenye faida kuliko ilivyokuwa awali.

Alisema mashine ya kukaushia mazao itawasaidia kuuza mazao yao wakati wowote wanapopata wateja tofauti na ilivyokuwa awali ambapo walikuwa wanawasubirisha wateja mpaka jua liwake kwa ajili ya kukaushia.





Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja Ayoub Mohmed Mahmoud aliyevaa suti nyeusi akiwa pamoja na Mwakilishi wa Tasaf kutoka Makao Makuu Mkangila Johnson katika uzinduzi wa kikao cha kujenga uweleaa kuhusu Mpango wa kunusuru Kaya Masikini kipindi cha Pili, Katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B uliyopo Kinduni **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# Wawakilishi, madiwani wapewa jukumu kutoa elimu ya TASAF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohmed Mahmoud, amewataka wawakilishi na madiwani kuwaelimisha wananchi juu ya mpango wa kunusuru kaya masikini katika maeneo yao hususani katika kufuata vigezo vya wananchi wanaopaswa kuwamo katika mpango huo.

Mkuu wa Mkoa aliyasema hayo wakati akizindua kikao kazi cha kujenga uwelewa kuhusu mpango wa kunusuru kaya masikini kipindi cha pili kwa viongozi , watendaji na wawezeshaji wa Mpango huo hafla iliyofanyika katika Wilaya ya Kaskazini 'B'.

Aliwataka watakaokuwa wanazihudumia kaya hizo kufanya kazi kwa uweledi ili lengo la mpango huo la kunusuru kaya masikini liweze kufanikiwa.

Alisema haipendezi kujihusisha katika vitendo vya ubadhirifu kwa kuingiza undugu katika kutekeleza majukumu yao na kuwaacha wahusika ambao wanapswa kuwamo katika mpango huo.

"Tunaomba muwe makini sana na kaya hewa, msije kujidanganya katika kufanya udanganyifu ikiwamo mhusika anaishi sehemu nyingine, lakini mtu anaenda kupiga picha nyumba ndogo iliyopo shambani ...hii haikubaliki kwani mfumo uliowekwa hivi sasa utawabaini watu hao na eneo hilo," alisema.

Alisema takwimu zinaonyesha kwamba utekelezaji wa mpango huo katika kipindi cha kwanza umesaidia kupunguza umasikini wa mahitaji ya msingi kwa kaya kwa silimia 10 na umasikini uliokithiri umepungua kwa asilimia 12 kwa kaya masikini sana.

Aidha, alisema utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya masikini pia umewezesha kaya walengwa kujikita kwenye shughuli za kukuza kipato na kujiimarisha kiuchumi, ikiwamo kujiingiza katika masuala ya ufugaji, kilimo, uvuvi na biashara ndogo.

Mkuu wa Wilaya wa Kaskazini 'B', Aboud Hassan Mwinyi, akimkaribisha mgeni rasmi ambae ni mkuu wa Mkoa huo, alisema watu hao watakaopatiwa mafunzo kwa ajili ya kuhudumia kaya maskini wafanye kazi zao kwa uhalisia ili kuepusha malalamiko.

Alisema yapo malalamiko kadhaa ya wananchi ambao walidai kuwa wapo watu ambao wanajiweza kuliko wao, lakini hawakuingizwa katika mpango huo mfuko huo wa kunusuru kaya masikini inaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Aliwataka washiriki tisa katika Wilaya ya Kaskazini 'B' watakaopatiwa mafunzo hayo kufanya kazi zao kwa uadilifu ili kuondoa malalamiko yaliyojitokeza katika kipindi cha kwanza.

Nae Mwakilishi wa TASAF kutoka Makao Makuu kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko huo, Mkangila Jonhson , alisema awamu ya tatu ya kipindi cha pili itatekelezwa kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2021-2023.

Alisema kutakuwa na mafunzo ya siku tano kwa watendaji ambapo kwa mwaka huu utambuzi utafanyika kwa njia ya kieletroniki ili kuondoa taswira mbaya kwa taasisi hiyo.

Mratibu wa TASAF Zanzibar, Saida Saleh Adam, alisema utekelezeaji wa Awamu ya Kwanza umetekelezwa kwa asilimia 70, hivyo asilimia 30 itakwenda kufanikiwa katika awamu ya tatu.

# Halmashauri kukusanya mil. 700/-

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kusini imepanga kukusanya zaidi ya Sh. milioni 700 kutoka vyanzo vya ndani vya mapato na kutumia zaidi ya bilioni moja na nusu kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kusini, kassim Abu Mtoro, wakati kiwasilisha ripoti ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2021/2022 kwa wajumbe wa baraza la madiwani wa Wilaya hiyo.

Alisema Sh. bilioni 1.5 zitatumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo, matumizi ya kawaida, miundombinu, masuala ya mtambuka pamoja na mishahara ya wafanyakazi.

Nao wajumbe wa baraza hilo walisema licha ya mafanikio waliopata katika sekta mbalimbali, lakini pia wanakabiliwa na matatizo yakiwamo usafiri, uhaba wa wafanyakazi hasa katika sekta ya kilimo, afya na elimu kwa walimu wa sayansi.

Walisema suala la elimu na walimu wa sanyansi ni changamoto kubwa katika shule zilizopo katika halmashauri hizo, hivyo ni vyema likaangaliwa kwa upana ili kupatiwa ufumbuzi.

"Changamoto ya walimu wa sayansi lipo katika shule nyingi, hivyo ni vyema tukawa na mikakati kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Elimu, wadau wa elimu ili kuona namna gani changamoto hii tunaitatua au kuutafutia ufumbuzi wa kudumu," alisema mmoja wa wajumbe.

Mkuu wa Wilaya ya Kusini, Rashid Makame Shamsi, aliwasisitiza madiwani na watendaji wa halmashauri hiyo kuwajibika ipasavyo na kujiepusha na matumizi mabaya ya fedha ili serikali iweze kutekeleza vyema malengo yake iliyojipangia.

Katika mkutano huo wajumbe wa baraza waliipitisha na kuridhia ripoti ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka mpya wa fedha

# Mikakati yatakiwa kukabili majanga

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imesema kuna umuhimu wa kuweka mikakati ya haraka ili kujipanga endapo yatatokea majanga ya kitaifa na kusababishwa kufunga kwa shule .

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Ali Khamis Juma ,alisema hayo wakati akichangia tathmini ya athari za kijinsia kwa wanafunzi katika kipindi cha kufungwa shule kufuatia mlipuko wa maradhi ya Corona mwaka 2020.

Alisema lazima jitihada zichukuliwe mapema ili kuwasaidia watoto kusoma kwa utulivu na kuwaepusha na matatizo mbalimbali yakiwamo ya mimba za mapema katika kipindi ambacho hawatakwenda shule.

Akitolea mfano kwa mwaka 2020 ambapo shule zilifungwa takribani miezi mitatu kutokana na janga la Corona hali iliyoleta athari kwa wanafunzi hata programu nzima ya ufundishaji kwa mwaka husika kutokana na wanafunzi kukaa nyumbani muda mrefu bila ya matarajio.

" Siku zote tumekuwa tukiangalia majanga ya mvua yaani vitu ambavyo tunajua vitatokea kimazingira, lakini hatukuwahi kuwaza kama itatokea janga ambalo litasababisha shule kufungwa , hivyo tunatakiwa lazima tuwe na mipango hii katika sekta ya elimu," alisema.

Mapema akiwasilisha ripoti hiyo, Mkuu wa Seksheni ya Stadi za Maisha kutoka Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Fatma Mbarak Hashim, alisema tathmini imeonyesha kuwa jumla ya wanafunzi 69 wameacha shule, wanafunzi 15 wamepata ujauzito, wanafunzi 2 ndoa za utotoni, wanafunzi 4 wa kike wamefanyiwa udhalilishaji wa kingono na wanafunzi 23 wamejiingiza katika ajira za utotoni.

Alisema tathmini hiyo imepatikana kufuatia ufatiti mdogo walioufanya katika mikoa yote mitano ya Zanzibar kwa shule 15 zikiwemo 10 za sekondari na 5 za msingi.

HABARI KIMATAIFA

# Treni yapinduka na kuua watu 11

**Cairo,** MISRI

AJALI ya treni iliyopinduka katika jijini la Banha Mkoa wa Qalyubia, imesababisha vifo vya watu 11 na wengine 98 kujeruhiwa, taarifa kutoka nchini hapa imeripoti.

Taarifa ya serikali imeeleza kuwa katika ajali hiyo, mabehewa manne yalipinduka na kusababisha taharuki na majeraha katika maeneo jirani, huku wakirejea picha za video zilizowekwa mtandaoni kuonyesha namna abiria walokuwa wakikimbia kutetea usalama wao.

Treni hiyo ilikuwa ikisafiri kwenda mji wa Nile Delta wa Mansoura kutoka mji mkuu wa Misri. Ilikuwa ni ajali mpya ya reli kuikumba nchi hiyo katika miaka ya hivi karibuni.

Ajali hiyo ilitokea Kaskazini mwa mji mkuu wa Misri Cairo hivi punde, wiki tatu baada ya treni mbili kugongana.

Kulingana na taarifa ya serikali, mabehewa manne ya treni kutoka Cairo kwenda Mansoura, kilomita 130 kaskazini mwa nchi, yalipoteza mwelekeo katika eneo la kilimo la Toukh. Sababu za ajali hazijajulikana.

"Watu kumi na moja wamefariki dunia na 98 wamejeruhiwa katika ajali ya treni huko Toukh", katika Delta ya Nile, kulingana na ripoti ya hivi punde kutoka kwa Wizara ya Afya.

Majeruhi 14 waliruhusiwa kutoka hospitali.

Magari mengi ya wagonjwa yalitumwa katika eneo la ajali, kulingana na Wizara ya Afya. Wachunguzi walitumwa huko kujaribu kujua sababu.

Rais wa Misri, Abdel Fattah al-Sisi, aliwaagiza wahandisi wa kijeshi kuchunguza ajali hiyo.

Kulingana na chanzo cha usalama, dereva wa treni na maofisa wengine wa treni wamekamatwa ili kuhojiwa. **VOA/RFI**



Picha ikionyesha treni iliyopata ajali na kusababisha vifo vya watu 11 na kujeruhi takribani 100, iliyotokea jiji la Delta, mji mkuu Cairo, Misri, juzi. **PICHA: XINHUA**

## Tembo waua mshukiwa ujangili

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

MSHUKIWA wa ujangili nchini hapa, amefariki baada ya kukanyagwa na tembo katika Hifadhi ya Taifa ya Kruger.

Mamlaka ya Hifadhi za Afrika Kusini (SANParks), juzi ilisema kuwa marehemu pamoja na wenzake wawili walikuwa wakikimbia askari walipoingia katika kundi la tembo.

SANParks ilisema kuwa mmoja wa washukiwa hao, alinaswa na askari na kuhadithia namna walivyokumbana na tembo hao.

Hakuwa na uhakika kama mwenzao amenusurika.

"Askari walimkuta akiwa amekanyagwa vibaya na tembo na kwa bahati mbaya akapoteza maisha kutokana na majeraha aliyoyapata," taarifa ya mamlaka ilieleza.

"Mshukiwa wa tatu inasemekana aliumizwa jichoni lakini ametoroka. Bunduki moja imepatikana…"

Mwaka 2019, mshukiwa wa ujangili wa faru alikanyagwa na tembo na kisha kuliwa na simba katika mbuga hiyo. **BBC**

## Huawei yakuza uwekezaji kibiashara

**Beijing,** CHINA

KAMPUNI ya mawasiliano ya Huawei, imebainisha mkakati wake wa kuboresha uwekezaji ili kukuza uthabiti katika biashara.

Pia imelenga kukabiliana na mvutano wa kijiografia, virusi vya corona na kuzuiwa kufanya biashara Marekani.

Taarifa hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa kampuni hiyo, Eric Xu, wakati akiwasilisha hotuba katika mkutano wa 18 wa wachambuzi wa kidunia ulioshirikisha zaidi ya watu 400.

Mkutano huo pia, ulijumuisha wachambuzi wa tasnia na wa kifedha, viongozi wa maoni na wawakilishi wa vyombo vya habari ulioanza Aprili 12 hadi 14.

"Uthibiti wa kibiashara ndio kanuni inayotuongoza. Tunataka kuongeza uimara wa biashara yetu yote na tangu mwaka jana tumekuwa tukifanya kazi kuboresha uwekezaji tukiwa na lengo hili," alisema Xu.

Xu alisema ripoti ya mwaka 2020 ya Huawei, ilionyesha mapato yaliyotokana na mauzo ya kampuni hiyo, mnamo 2020 kufikia CNY891.4 bilioni.

"Tunatafuta fursa mpya za kibiashara katika sekta ya programu. Tunapopata kitu kinachotufaa, tutaongeza uwekezaji ili kuongeza ushiriki wa huduma za program katika vyanzo vyetu vya mapato," alisema Eric Xu.

Novemba mwaka 2018, Huawei iliwekeza kiasi cha dola za kimarekani bilioni mbili katika kuboresha uwezo wao wa uhandisi wa programu.

## Chad lawashikilia waasi

**Mao,** CHAD

CHAD inaendelea kushuhudia mdororo wa usalama, siku mbili baada ya mapigano makali kutokea kati ya vikosi vya serikali na waasi wa kundi la Front for Alternation and Concord in Chad (FACT), mwishoni mwa wiki.

Mapigano hayo yalitokea Kaskazini mwa mji wa Mao, katika Mkoa wa Kanem, zaidi ya kilomita 300 kutoka mji mkuu Ndjamena.

Kundi la waasi wenye silaha, ambalo liliokea katika ngome yake kuu nchini Libya, liliingia nchini Chad Aprili 11, kwa lengo la kumtimua Idriss Deby, mamlakani.

Jeshi lilitangaza kuwa kati ya waasi 250 na 300 wameuawa, na waasi wengine 150 wamekamatwa, ikiwa ni pamoja na kiongozi wa chama cha siasa ambaye aliamua kujiunga na kundi la waasi miaka michache iliyopita.

Kundi lingine la waasi lilielekea upande wa Magharibi na hadi juzi jioni lilikuwa halijaonekana.

Serikali ya Uingereza ilisema msafara wa FACT ulikuwa ukielekea Kusini Magharibi, kuelekea mji mkuu N'Djamena na ulizidi mji wa Faya, kwenye umbali wa kilomita 770 (maili 478) na mji wa N'Djamena.

Msafara mwingine ulionekana ukikaribia mji wa Mao, karibu kilomita 220 Kaskazini mwa N'Djamena, serikali ya Uingereza ilisema kwenye tovuti yake ya ushauri kuhusu safari.

Hata hivyo upinzani ulisema kuwa hakuna uchaguzi uliofanyika nchini Chad. **RFI**

## HABARI MICHEZO



# NEYMAR SASA AKARIBIA KUSANI MKATABA MPYA

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR anakaribia kusaini mkataba mpya na mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa Canal+.

Kwa muda mrefu, Neymar amekuwa akitajwa kwamba, anataka kurudi tena kujiunga na Barcelona baada ya kuondoka kule Camp Nou kwa ada iliyoweka rekodi mwaka 2017.

Majaliwa ya Neymar yalikuwa shakani kuendelea kuwapo hapo jijini Paris wakati uvumi ukiendelea kumhusisha na mpango huo wa kuondoka.

Lakini sasa Paris Saint-Germain wapo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumuongezea mkataba mpya nyota huyo wa kimataifa wa Brazil.

Neymar mwenyewe wiki iliyopita alinukuliwa akisema kwamba anataka kuendelea kukaa na klabu hiyo, hasa baada ya kufuzu hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# Tuchel ajipigia debe mkataba mpya Chelsea

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel amesema tayari anahisi kama vile ni sehemu ya familia ya Chelsea na amefungua milango kwa ajili ya kusaini mkataba mpya kama klabu hiyo inaona anastahili kubakia hapo.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 47, alichukua mikoba ya Frank Lampard hapo Stamford Bridge Januari kwa mkataba wa awali wa miezi 18 ambao unaweza kuongezwa.

Amefurahia mwanzo mzuri wa maisha hapo Chelsea, akishinda mechi 13, sare nne na kupoteza mbili katika mechi zake za kwanza 19 akiwa kama kocha mkuu.

Na ameiwezesha Chelsea kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na fainali ya Kombe la FA, na pia kuwa na matumaini ya kumaliza kwenye nne bora ya Ligi Kuu.

Tuchel amebainisha kwamba, alikuwa na woga wa namna ya kupata mafanikio hapo London na sasa yupo tayari kuongeza mkataba.

"Nilikuwa na mawazo mengi, lakini baadaye ninasema mambo yatabadilika na naweza kuendelea kukaa hapa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Huwa napenda mafanikio, nataka matokeo bora kadiri ninavyoweza. Kama nastahili kubaki hapa, nataka kukaa kwa muda mrefu zaidi.

"Nahisi kama familia ya Chelsea. Tumekuwa na wakati mzuri wa kuvutia hapa pamoja na timu na nataka kupambana zaidi.

"Hivyo sijali watazungumza nini kuhusu mkataba wangu. Nahitaji kustahili kukaa hapa kwa muda mrefu zaidi, hivyo nitakaa sana."





# Conte ataka zaidi kutoka kwa Eriksen

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amesema bado kuna nafasi ya kuimarika zaidi kwa Christian Eriksen, lakini alimsifia kiungo huyo kwa kiwango kizuri wakati Inter ikipata pointi moja Jumapili.

Eriksen alionekana angeondoka Inter katikati ya msimu huu baada ya Ofisa Mtendaji wa klabu hiyo, Giuseppe Marotta, kubainisha kwamba amemuweka kwenye orodha ya wachezaji wanaoondoka.

Nyota huyo wa zamani wa Tottenham amerudi kwenye mipango ya Conte na Jumapili aliiwezesha Inter kupata sare ya bao 1-1 dhidi ya Napoli baada Samir Handanovic kujifunga mwenyewe kipindi cha kwanza.

Alifunga bao dakika ya 24 kwa shuti na kuweza kuwafanya Inter kupata pointi hiyo moja kwa bao la kusawazisha.

Matokeo hayo yalimaliza umwamba wa Nerazzurri hao wa kushinda mech 11 mfululizo kwenye Serie A, ingawa wamebaki kwenye nafasi nzuri ya kushinda taji la ligi hiyo kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2009-10.

Conte bado anataka zaidi kutoka kwa Eriksen, lakini aliridhishwa na kuimarika kwake katika mechi za hivi karibuni.

# Zidane: Tutapambana LaLiga hadi kieleweke

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane ameiambia Real Madrid kuendelea "kupambana hadi kifo" baada ya kutoka sare ya bila kufungana na Getafe na hivyo kuwaweka kwenye wakati mgumu katika mbio zao za ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Iliitoa Atletico Madrid kileleni mwa msimamo kwa pointi moja kwa ushindi wao wa mchezo wa El Clasico dhidi ya Barcelona wiki iliyopita, lakini kikosi hicho cha Zidane kilisindwa kupata pointi tatu pale kwenye dimba la Coliseum Alfonso Perez, Jumapili.

Golikipa wa Madrid, Thibaut Courtois, aliokoa hatari sita kwenye lango lake dhidi ya Getafe.

Baada ya mchezo huo, Zidane aliwaambia waandishi wa habari: "Tulicheza kwa kiwango cha juu kabisa. Ni sare, lakini tunaendelea kupambana. Hilo halitaishia hapa.

"Kuna mechi nyingi, lakini timu itakayokwenda kushinda itahitaji kupata ushindi kwa mechi zake zote na sisi tutafanya kila tunaloweza, hasa kwa wachezaji wangu.

"Tunatakiwa kuwa kwenye ubora wetu. Hatuna namna nyingine, kwani tukitaka kushinda taji hili lazima tushinde kila mchezo uliopo mbele yetu."

Ushindi wa Atletico wa mabao 5-0 dhidi ya Eibar kwenye mchezo wa mapema Jumapili, maana yake inaongoza msimamo kwa tofauti ya pointi tatu dhidi ya Madrid waliopo nafasi ya pili na tano dhidi ya Barcelona waliopo nafasi ya tatu, lakini wana mchezo mmoja mkononi.





# IHEANACHO ALIPANIA KUTWAA KOMBE LA FA

**LONDON,** England

KELECHI Iheanacho nyota wa Klabu ya Leicester City, amewashukuru mashabiki kwa sapoti yao na kuahidi kuendelea kupambana kwa ajili ya mafanikio ya timu hiyo.

Usiku wa kuamkia jana kwenye Uwanja wa Wembley, Iheanacho alikuwa shujaa baada ya kutupia bao la ushindi dakika ya 55 katika nusu fainali ya Kombe la FA mbele ya Southampton ambayo imefungashiwa virago katika kombe hilo.

Ushindi huo unaipa nafasi Leicester City kutinga hatua ya fainali na itakutana na Chelsea ambayo iliitoa Manchester City katika hatua ya nusu fainali.

Ikiwa na miaka 137, Leicester City haijawahi kushinda taji la FA licha ya kufika katika fainali zake mara nne ila wana taji la Ligi Kuu England ambalo walilitwaa miaka mitano iliyopita.

Nyota huyo mara baada ya mchezo huo, aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram: "Asanteni sana kwa sapoti yenu mashabiki wenu kwa kila mmoja kutoka nyumbani, ninawashukuru kwa mara nyingine tena.

"Nina amini kwamba tutaonana kwenye fainali ila endeleeni kukaa salama huko mlipo."

# De Bruyne aipa pigo Man City

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City itamtathmini Kevin De Bruyne kugundua ukali wa jeraha la kiungo huyo kabla ya safari ya Jumatano kuivaa Aston Villa.

De Bruyne aliumia wakati wa mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Chelsea Jumamosi na jeraha la kifundo cha mguu baada ya kugongana na N'Golo Kante.

Ilikuwa ni changamoto isiyo na hatia kutoka kwa kiungo wa Chelsea, lakini De Bruyne alionekana kuumia mguu wake na hakuweza kuendelea, na Phil Foden alichukua nafasi yake baada ya dakika 48.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji atafanyiwa vipimo Jumapili, lakini bosi wa City, Pep Guardiola, alitoa makadirio yake ya awali kuwa jeraha ni la kutisha baada ya mchezo kumalizika.

Alipoulizwa juu ya taarifa mpya, Guardiola aliiambia Manchester Evening News: "Sijui, lakini ana maumivu.

"Jumapili tutafanya vipimo na madaktari, lakini haionekani vizuri. Tutaona."

De Bruyne alikosa michezo saba Januari na Februari kwa sababu ya jeraha la nyama za paja, pamoja na kutokuwapo kwenye michezo miwili mwaka 2019, hana historia ya shida ya kifundo cha mguu.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LIVERPOOL SASA YAFUNGIA KAZI USAJILI WA DEMBELE

●●● Ni mpango wa kuja kumrithi Mane ambaye amekuwa na msimu mbaya, hivyo atauzwa majira...

**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool imejiandaa kutumia fedha nyingi kumsajili winga wa Barcelona, Ousmane Dembele, kama mbadala wa straika Msenegal Sadio Mane katika kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

**Umekuwa msimu wa kukatisha tamaa kwa Mane, ambaye amefunga mabao 12 tu kwenye mashindano yote na matano tu tangu mwanzoni mwa mwaka huu, wakati kikosi hicho cha kocha Jurgen Klopp kikitolewa kwenye mashindano kwa kila kombe.**

Kwa mujibu wa ESPN, Liverpool inafikiria kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal mwenye umri wa miaka 29, katika msimu huu wa majira ya joto licha ya mkataba wake kubakisha miaka miwili kumaliza.

Kulingana na ripoti za Fichajes. net huko Hispania, Dembele ndiye mtu anayekusudiwa kuchukua nafasi yake.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, Dembele mwenye umri wa miaka 23, amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake na Barcelona, lakini bado hajasaini nyongeza aliyopewa.

Wiki iliyopita Dembele mwenyewe alibainisha kwamba, bado hajui kinachoendelea kuhusu kusaini mkataba mpya, lakini alisema ana matumaini mambo yatakwenda kama yalivyopangwa.

Kocha wa Barcelona, Ronald Koeman, mapema wiki hii alinukuliwa akisema kuwa anataka Dembele aendelee kuwa kwenye kikosi hicho, kwa sababu bado ana mipango naye.

Dembele mara kadhaa ameweka wazi kuwa hana mpango wa kuondoka Barcelona, licha ya klabu za Manchester City na Manchester United kujaribu kutaka kumsajili.

Msimu huu Dembele umekuwa bora zaidi kwake baada ya kutoka kupona majeraha yaliyomuweka nje ya dimba kwa kipindi kirefu.

## ZISIKUPITE

### MESSI HAJAPEWA OFA

BARCELONA haijampatia ofa mpya Lionel Messi, 33, ambaye mkataba wake na klabu hiyo unakamilika msimu huu. ***(Marca)***

### MBAPPE KUBAKI PSG

KOCHA wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, ana matumaini mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 22, atakubali kufikia mkataba mpya na klabu hiyo. ***(Goal)***

### LACAZETTE MKATABA BADO

ALEXANDRE Lacazette amesema uamuzi kuhusu mkataba mpya Arsenal "si wangu pekee", wakati mkataba wa sasa wa mshambuliaji huyo wa Ufaransa aliye na umri wa miaka 29, ukitarajiwa kukamilika mwaka 2022. ***(Mirror)***

### KEAN HAITAKI EVERTON

WAZO la mshambuliaji wa Italia, Moise Kean, 21, kurejea Everton baada ya kumaliza muda wa kucheza kwa mkopo kule PSG ni "ngumu kufikiria", kwa mujibu wa ndugu yake, Giovanni. ***(Tuttosport)***

### NAGELSMANN HAENDI BAYERN

KOCHA wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann amekaririwa kuwa hajafanya mazungumzo na Bayern Munich juu ya kumbadilisha Hansi Flick kama kocha wao. ***(Goal)***

### INTER YAMTAKA EMERSON

KLABU ya Inter Milan inataka kumsajili mchezaji, Emerson Palmieri, 26 kutoka Chelsea. ***(Todofichajes)***

### SZCZESNY HAONDOKI JUVE

GOLIKIPA wa Poland na mlinda mlango wa zamani wa Arsenal, Wojciech Szczesny, 31, hataondoka Juventus kujiunga na Tottenham msimu huu. ***(Goal)***

### IBRAHIMOVICH KUSAINI MPYA

MKURUGENZI wa AC Milan, Ricky Massara, amesema anatarajia klabu hiyo itafikia mkataba mpya na mshambuliaji Zlatan Ibrahimovic, 39, na ana "imani" mlinda mlango wa Italia Gianluigi Donnarumma, 22, na kiungo wa kati wa Uturuki, Hakan Calhanoglu mwenye miaka 27, watatia saini mkataba mpya katika klabu hiyo ya Serie A. ***(DAZN, via Football Italia)***

### ABRAHAM AGOMBEWA

LEICESTER na West Ham zinawania kumsajili straika wa Chelsea na England, Tammy Abraham, 23, baada ya kutokuwa na namba ya kudumu pale 'The Blues'. ***(Guardian)***

### ANCELOTTI AMTAKA OLSEN

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, anataka kumsajili golikipa wa Sweden, Robin Olsen, 31, na hivyo kubadilisha mkataba wake wa mkopo kutoka AS Roma kuwa wa kudumu. ***(Liverpool Echo)***

## Simbu sasa hakuna kulala Olimpiki 2021

**Na Shufaa Lyimo**

MWANARIADHA Alphonce Simbu, amesema hana muda wakupoteza kwa sasa na amekuwa akiendelea na mazoezi makali kujiandaa na michuano ya Olimpiki 2021 inayotarajiwa kufanyika Julai, mwaka huu Tokyo, Japan.

Akizungumza na gazeti hili jana, mwanariadha huyo alisema anafanya mazoezi ya kukimbia kwa muda mrefu ili kuhakikisha anakwenda kufanya vizuri katika mashindano hayo ambayo anaamini yatakuwa na ushindani mkubwa.

Aidha, Simbu aliwaomba Watanzania kuzidi kumuombea ili aende kuiwakilisha vizuri nchi ikiwamo kukitangaza kipaji chake kupitia mashindano hayo, huku akiwataka wachezaji ambao mpaka sasa bado hawajafuzu kushiriki mashindano hayo kuongeza juhudi.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Riadha Tanzania (RT), John Bayo, aliwaomba Watanzania waiunge mkono timu ambayo inakwenda kushiriki mashindano hayo, ili wachezaji waweze kupata unafuu wa kufanikisha safari yao hiyo.

## Pawasa: Ni kazi kazi kuelekea BSAFCON

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa Soka la Ufukweni, Boniface Pawasa, amesema kikosi chake kinaendelea na mazoezi magumu kwa ajili ya kujindaa na mashindano ya Kombe la Mataifa Afrika (BSAFCON) yanayotarajiwa kufanyika Mei 23-29, mwaka huu huko Dakar, Senegal.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Pawasa alisema ameamua kuanza kambi mapema kwa lengo la kuwaweka sawa wachezaji wake ambao wanajiandaa kukabiliana na kibarua hicho kizito cha kuipeperusha vema bendera ya Tanzania kimataifa.

Alisema mazoezi ambayo anawapa wachezaji wake yatawasaidia kwa kiasi kikubwa kutoa ushindani katika mashindano hayo, na kwamba kila mchezaji ameahidi kwenda kufanya vizuri ili kuitangaza vema Tanzania.

Aliwashukuru Watanzania pamoja na wadau mbalimbali wa mchezo huo kutokana na ushirikiano ambao wanawaonyesha kwa kujitokeza kwa wingi kushuhudia viwango vinavyoonyeshwa na wachezaji pindi timu hiyo inapokuwa inacheza, jambo ambalo linazidi kumpa matumaini.

# ORLANDO YANYEMELEA USAJILI WA ONYANGO SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Orlando Pirates ya Ligi Kuu Afrika Kusini, imetajwa kumtaka beki kisiki wa Simba, Mkenya Joash Onyango (pichani), kutokana na kuvutiwa na kiwango chake kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Haji Manara, amesema alipigiwa simu na mtu aliyejitambulisha kuwa ni kiongozi wa klabu hiyo na kumuulizia kama anaweza kumsajili.**

"Niwaibie siri, jana (juzi) Meneja wa Orlando Pirates alinipigia simu na kuniambia wamevutiwa na Onyango. Kaniuliza wakimtaka mchezaji huyo ofa yake bei gani na mimi nikawatania labda walete dola milioni moja," alisema Manara.

Manara alisema kwa sasa hawezi kutaja kiasi halisi cha gharama ya Onyango, lakini hawezi kuuzwa kwa pesa ndogo kwa sababu ni mmoja wa mabeki ghali na bora Afrika kwa sasa.



"Hivi majuzi tu kachaguliwa kuwa mmoja wa mabeki bora Afrika unafikiri atauzwa bei gani?" Alisema.

Katika hatua nyingine, Manara alisema kuwa kwa sasa Simba imekuwa ikifuatiliwa si Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati tu, bali Afrika nzima na wachezaji wake pia wamekuwa wakifuatiliwa kwa karibu na klabu zote Afrika.

"Kuna mtaalam mmoja nchini Kenya ameandika kuwa Simba inaweza kuwa ni alama ya klabu zote za Ukanda wa Afrika Mashariki na ni kweli kwa sababu uwekezaji umefanyika. Myonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni, bila Mohamed 'Mo' [Dewji], sisi wanachama na mashabiki wa Simba tungeweza kumlipa mchezaji Luis Miquissone? Tunaweza kumlipa Chama?" Alihoji.

Amebainisha kuwa wachezaji wa Simba, benchi la ufundi na wafanyakazi wote wa klabu ya Simba mishahara yao kwa pamoja inazidi kiasi cha Sh. milioni 300 kwa mwezi.

"Mo amekuwa akilipa mishahara ya wafanyakazi wote wa Simba, kuanzia wachezaji, benchi la ufundi hadi sisi, Sh. milioni 300 kila mwezi, ni kama wizara tu. Ndiyo maana ninawaambia Simba kwa sasa ni dude kubwa. Halafu kuna mtu anakuja anamsema vibaya Mo. Nadhani hajui nini anachokisema," alisema Mkuu huyo wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba.

**TUPO TAYARI...**



Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi na Kiungo wa timu hiyo, Haruna Niyonzima (Kulia), wakizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Gwambina FC itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa leo. **PICHA: YANGA**

# *Azam yazipotezea Simba, Yanga mbio ubingwa*

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema hawana muda wa kuwatazama Simba na Yanga wanafanya nini zaidi ya wao kuhakikisha wanaonyesha kiwango bora na kutafuta matokeo kwa kila mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Vivier alisema malengo makubwa ni kupambana kutafuta nafasi mbili za juu, ubingwa au nafasi ya pili ambazo zitawafikisha katika malengo yao ya kushiriki michuano ya kimataifa kwa msimu ujao.

Alisema wanapambana kuhakikisha wanashinda mechi zao bila kuangalia wanaowafuata na waliopo juu yao wanafanya nini, zaidi ya kupigania kumaliza michezo yao kwa kupata ushindi.

"Tunahitaji kushinda mechi zetu zote, bila ya kuangalia waliokuwa juu, kuhakikisha kila mechi kwetu tunahitaji kupata matokeo mazuri ili kufikia malengo yetu ya kumaliza tukiwa katika nafasi mbili za juu," alisema Vivier.

Alisema wanaendelea vizuri na maandalizi yao huku wakifanyia kazi upungufu unaojitokeza katika kila mechi ikiwamo safu ya ulinzi kutoruhusu mabao na washambuliaji kutumia vema nafasi wanazozitengeneza kupata mabao.

"Baada ya kupata ushindi dhidi ya JKT Tanzania, sasa tunaendelea na maandalizi ya mechi yetu dhidi ya Dodoma jijini kuhakikisha tunapata ushindi na kufikia malengo yetu," alisema Vivier.

Azam ambayo ipo nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi zake 50 zilizotokana na michezo 26, keshokutwa, Alhamisi itashuka katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma kuvaana na Dodoma Jiji FC kwenye mwendelezo wa ligi hiyo.

# Michezo

Jumanne Aprili 20, 2021

Nipashe




## Orlando yamnyemelea Onyango wa Simba

HABARI UK.23

## Yanga kumshusha kocha wa Al Merrikh

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga wakati wowote kuanzia leo, huenda ikamtangaza aliyekuwa Kocha Mkuu wa Al-Merrikh ya Sudan, Nasreddine Nabi, kuwa Kocha Mkuu mpya kuchukua mikoba ya Cedric Kaze aliyetimuliwa Machi 7, mwaka huu.

Habari za ndani kutoka Klabu ya Yanga, zimeeleza kuwa kocha huyo huenda akawasili muda wowote kuanzia leo kuungana na bechi la ufundi lililopo kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea na kuna uwezekano wa kutambulishwa kabla ya mechi dhidi ya Azam FC itakayochezwa Jumapili wiki hii.

Taarifa zinasema kuwa awali kulikuwa na majina mawili ya waliotakiwa kuinoa Yanga ambao wote walikuwa Al-Merrikh, nao ni Mserbia Miodrag Jesic na Mtunisia huyo, lakini Nasreddine akakubalika zaidi na kurithi mikoba ya Didier Gomes da Rosa baada ya kujiunga na Simba.

Mtunisia huyo aliiogoza Al Merrikh kwenye mechi tatu tu za Ligi ya Mabingwa Afrika na alipoteza kwa mabao 3-0 ugenini dhidi ya Al Ahly ya Misri, mabao 4-1 nyumbani dhidi ya AS Vita na suluhu ya bila kufungana dhidi ya Simba nyumbani, matokeo ambayo yalimsababishia kutimuliwa saa chache baada ya mechi kumalizika na nafasi yake kuchukuliwa na Lee Clark..

Alipoulizwa juu ya ujio wa kocha huyo, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema: "Hakuna kitu kama hicho, kocha wetu sisi ni Juma Mwambusi ambaye anaendelea na kazi. Hakuna kocha yeyote ambaye tunamtegemea kuja kwa sasa na kama kuna lolote jipya, basi tutawaambia na wala si kama hivyo mnavyosema ninyi".

**NIMEHAMA YANGA...**



Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, akicheza muziki wa Singeli katika Studio za Wasafi FM na msanii maarufu wa miondoko hiyo, Dulla Makabila (kushoto), baada ya kutangaza rasmi kubadili ushabiki wake kutoka Yanga na kuwa shabiki kindakindaki wa Wekundu wa Msimbazi hao kuanzia jana. Kushoto ni mchambuzi wa soka wa Wasafi FM, Edo Kumwembe. Utambulisho wa shabiki huyo ulienda sambamba na uzinduzi moto wa wimbo mkali wa Singeli wa kuishabikia Simba. **MPIGAPICHA WETU**

# LIGI YA MABINGWA ULAYA VIPANDE VIWILI

**Nyon, USWISI**

### ●●● Madrid, Barcelona, Man United, Liverpool, Man City, Juve, Inter, Chelsea, zatangaza kujitoa UEFA huku...

SHIRIKISHO la Soka barani Ulaya (UEFA), jana limefanya mkutano kuhusu mgogoro wa mpasuko mkubwa saa kadhaa baada ya klabu kubwa 12 kuushtua ulimwengu wa soka kwa kutangaza kuanzishwa kwa michuano mipya ya Ulaya maarufu kama European Super League (ESL).

Klabu ambazo tayari zimetanga uamuzi huo kwa England ni Liverpool, Arsenal, Chelsea, Manchester City, Manchester United na Tottenham, wakati kwa Hispania ni Real Madrid, Barcelona, Atletico Madrid, huku kwa Italia zikiwa ni AC Milan, Inter Milan na Juventus.

ESL imeeleza kuwa klabu hizo anzilishi zimekubali kuanzisha "michuano mipya ya katikati ya wiki" wakati timu hizo zikiendelea kushindana katika ligi zao za ndani kama kawaida huku pia ikieleza kwamba inapanga kuanzisha michuano ya wanawake mapema iwezekanavyo baada ya mashindano hayo ya wanaume kuanza.

Benki ya Uwekezaji ya Marekani JP Morgan (JPM.N) imeithibitishia Reuters kwamba inafadhili ligi mpya, ambayo inajumuisha klabu kama Real Madrid na Manchester United na ni mpinzani wa mashindano ya UEFA ya Ligi ya Mabingwa.

JP Morgan inatoa ruzuku ya Yuro bilioni 3.5 kwa klabu anzilishi kutumia kwenye miundombinu na kuziba mapengo yaliyotokana na athari za janga la COVID-19.

Vita vikali vya kudhibiti mchezo huo na mapato ya mabilioni ya dola zake viliingia katika hatua mpya na barua iliyotumwa na klabu 12 kwa UEFA Jumatatu ambapo walisema watachukua hatua za kisheria katika mahakama ambazo hazina jina kulinda masilahi yao kama wanavyoweka kuhusu ligi hiyo.

Mpasuko huo umekuwa ukikosolewa vikali na mamlaka za soka, mashirika ya mashabiki na wanasiasa kote Ulaya ambao wanasema inatia utajiri na nguvu ya wasomi wadogo wa klabu.

Klabu zilizojitenga zitahakikishiwa nafasi za kila mwaka kwenye mashindano hayo- tofauti na Ligi ya Mabingwa ya UEFA, ambayo inahitaji timu kufuzu kupitia ligi zao za ndani.

> **"Kuundwa kwa Super League kunakuja wakati janga la virusi vya corona ulimwenguni limeongeza kasi ya kuyumba kwa mtindo wa uchumi wa mpira wa miguu uliopo Ulaya," klabu zilisema katika taarifa yao ya uanzishaji.**

Hesabu za akaunti za mwisho za Barcelona, moja miongoni mwa klabu 12 anzilishi za ESL, zilionyesha deni kubwa la zaidi ya euro bilioni 1.4 na deni halisi la milioni 488 ambapo klabu hiyo ilikubaliana kupunguza malipo ya wachezaji kwa muda mfupi mwaka jana na ililazimika kuchelewesha malipo kwa wachezaji kwa Desemba.

UEFA iko tayari kupambana na waliojitenga, na Jumapili ilisema kwamba "itazingatia hatua zote zinazopatikana kwetu, katika ngazi zote, za kimahakama na michezo ili kuzuia hilo kutokea".

UEFA pia ilisema klabu zinazohusika "zitapigwa marufuku kucheza kwenye mashindano mengine ya ngazi yoyote ya nyumbani, Ulaya au duniani, na wachezaji wao wanaweza kunyimwa fursa ya kuwakilisha timu zao za taifa".

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

7 70856 541002 >